# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Novemba 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580385

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 9

**POLISI** Zanzibar wakiri kumshikilia kigogo wa juu ACT- Wazalendo



UKURASA 3

**NDEGE** kubwa ya aina yake yatua Dodoma kwa mara ya kwanza

UKURASA 3

**RIPOTI MAALUM**

# Machinga wanavyoweka rehani maisha ya watembea kwa miguu

**KILA** baada ya sekunde 24 kifo kinatokea, yadaiwa kuwa chanzo cha ajali za barabarani... *Endelea Ukurasa wa 4*



## Viongozi, wagombea upinzani watoa tamko rasmi kupinga matokeo

UKURASA 2

Viongozi wa vyama vya upinzani vya ACT-Wazalendo na CHADEMA, wakionyesha mshikamano jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutoa tamko la pamoja kuhusu uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 27 na 28.2020. Kutoka kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa ACT Bara, Dorothy Semu, Kiongozi Mkuu wa ACT, Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, aliyekuwa Mgombea Urais wa Chadema, Tundu Lissu na mgombea mwenza, Salum Mwalimu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JPM kukabidhiwa hati leo

UKURASA 2'




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **AZAM FC YALIA KUKOSA BAHATI** UK.24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Magufuli kukabidhiwa cheti cha ushindi leo

**Na Waandishi Wetu,**
DODOMA

RAIS Mteule wa Tanzania, Dk. John Magufuli, anatarajiwa kukabidhiwa cheti cha ushindi wa kiti hicho jijini Dodoma leo.

Magufuli ambaye ni Mgombea kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) pamoja na Makamu wa Rais Mteule, Samia Suluhu Hassan, watakabidhiwa cheti hicho kwenye ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) zilizoko Njedengwa jijini hapa.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, cheti hicho cha ushindi kinakabidhiwa leo kwa Dk. Magufuli ambaye ameshinda kwa kupata kura 12,516,252 kati ya kura halali 14, 830,195 zilizopigwa.

Katika kinyang'anyiro hicho, nafasi ya pili ilishikwa na Tundu Lissu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambaye amepata kura 1,933,271.

Wagombea wengine ambao idadi ya kura zao zipo kwenye mabano ni pamoja na Leopold Mahona wa NRA(80,787), John Shibuda wa ADA-TADEA (33,086), Muttamwega Mgaywa wa SAU (14,922), Cecilia Mwanga wa Demokrasia Makini (14,556), Yeremia Maganja wa NCCR-Mageuzi (19,966), Profesa Ibrahim Lipumba wa CUF(72,885), Philipo Fumbo wa DP (8,283), Bernard Membe wa ACT-Wazalendo (81,129) na Queen Sendiga wa ADC(7,627).

Wengine ni Twalib Kandege wa UPDP (6,194), Hashim Rungwe wa CHAUMMA (32,878), Khalfan Mazrui wa UMD (3,721) na Seif Seif wa AAFP (4,635).

Katika hatua nyingine, wagombea tisa waliokuwa kwenye kinyang'anyiro hicho kati ya 15, wamempongeza Dk. Magufuli kwa ushindi huo huku wakisema wako tayari kushirikiana naye.

Wagombea hao ni kutoka vyama vya AAFP, Demokrasia Makini, DP, UPDP, SAU, NRA, ADC, UMD na NCCR-Mageuzi.

Wamesema anguko la wapinzani ni la haki kutokana CCM kujipanga na kutekeleza sera zao kikamilifu.

Mgombea wa UMD, Khalfan Mazrui, alisema uchaguzi mkuu ulikuwa wa haki na amani, hivyo ushindi alioupata Dk. Magufuli ni halali. "Kikwazo cha nchi za Afrika cha kutokukubaliana na matokeo ni donda sugu, huwa ni vigumu kukubaliana na ushindi, ni lazima aseme ameonewa," alisema.

Alisema vyama vya upinzani vimeponzwa na wabunge waliotangulia kwa sababu walishindwa kutekeleza sera walizojinadi katika majimbo yao na kusababisha Watanzania kushindwa kuwachagua wapinzani na kukipa nafasi chama tawala kuendelea kupata ushindi kutokana na uwekezaji wa maendeleo kiloufanya.

"Wakati mwingine tulikuwa tunakata tamaa hata kufanya kampeni kwa sababu ukipita katika maeneo, watu wanajaa kwa sababu ya mwonekano wako, wanakuja kusikiliza sera zako lakini hawakupigii kura kwa sababu wanaona maendeleo yaliyofanywa na yanayoendelea kutekelezwa," alisema.

Yeremia Maganja wa NCCR-Mageuzi, aliwapongeza watendaji wote wa NEC kutokana na kuendesha uchaguzi wa haki.

Alisema wamekubaliana kwa kauli moja kumuunga mkono Dk. Magufuli na kuwaasa wananchi kuwa watulivu na wasikubali kudanganywa kufanya mambo kinyume cha taratibu za kisheria.

Mgombea wa DP, Philipo Fumbo, alisema katika mchakato mzima walikuwa wagombea 15 na nafasi iliyokuwa inawaniwa ni moja, hivyo haiwezekani wakashinda wote, ni lazima apatikane mmoja na wananchi wameona anayefaa kuwaongoza ni Dk. Magufuli.

Alisema wapo tayari kufanya kazi na serikali itakayokuwapo madarakani kwa sababu lengo lao lilikuwa ni kuwatumikia wananchi na mchango wao unaweza kutumika hata wakiwa nje ya urais.

Mgombea wa NRA, Leopold Mahona, aliipongeza NEC kwa maandalizi mazuri yaliyopelekea uchaguzi kufanyika kwa amani na utulivu.

Mgombea wa Demokrasia Makini, Cecilia Mmanga, aliwaomba Watanzania kumuunga mkono Rais Mteule kwa kufanya kazi kwa kuwa uchaguzi umekwisha na mshindi amepatikana.

Mgombea wa UPDP, Twalib Kadege, alisema katika kipindi chote cha kampeni, Dk. Magufuli alitumia mikutano yake kueleza alichokifanya na anachotarajia kukifanya bila ya matusi wala jazba na wananchi wamemwelewa.

Mgombea wa ADC, Queen Sendiga, alisema katika shindano lazima mshindi apatikane, hivyo wao wamekubaliana na ushindi wa Dk. Magufuli na wanaahidi kushirikiana naye katika shughuli za ujenzi wa taifa.

■**Imeandikwa na Augusta Njoji na Renatha Msungu**



Mafundi wakitoa maji kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa kingo za Mto Ng'ombe, eneo la Sinza Shekilango, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Upinzani watoa tamko matokeo ya uchaguzi

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wakuu wa vyama vya CHADEMA na ACT-Wazalendo pamoja na wagombea wao wa nafasi ya urais, wametoa tamko la pamoja la kutokubali matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Jumatano iliyopita.

Matokeo yanayopingwa na viongozi hao ni yaliyotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Akisoma tamko la pamoja lililotokana na vikao vyao vilivyokaa juzi na jana, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alidai kilichofanyika Oktoba 28, yaani Jumatano, hakina sifa wala uhalali wa kuitwa uchaguzi mkuu.

"Kwa umoja wetu, tunaamini kilichofanyika Oktoba 28, hakina sifa wala uhalali wa kuitwa uchaguzi mkuu bali unyang'anyi na uporaji wa kutumia nguvu wa haki ya Watanzania ya kuchagua viongozi kwa njia ya demokrasia," alisema.

Tamko hilo lilitiwa saini mbele ya waandishi wa habari na Mbowe na Tundu Lissu (Mgombea Urais wa CHADEMA) huku upande wa ACT-Wazalendo ukiwakilishwa na Zitto Kabwe, Kiongozi Mkuu wa chama hicho aliyemwakilisha pia Mgombea Urais wa Zanzibar kupitia chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad.

Katika tamko lao hilo, viongozi hao wa vyama vya upinzani walisema wamekubaliana kudai kuitishwa upya kwa uchaguzi mkuu haraka iwezekanavyo.

"Tunahitaji kuvunjwa kwa NEC na ZEC na kuundwa tume huru ya kusimamia uchaguzi," alisema Mbowe alipokuwa anasoma tamko lao hilo.

Vyama hivyo pia vimewatangazia wanachama wake, watetezi wa haki za binadamu na wote ambao hawajakubaliana na uchaguzi huo, kushiriki katika kile walichokiita maandamano ya amani yasiyo na kikomo kuanzia kesho hadi hapo madai yao yatakapotekelezwa.

Viongozi hao pia wametoa wito kwa taasisi za kikanda, za kimataifa, nchi rafiki na jumuiya ya kimataifa kutotambua uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 uliokipa ushindi mkubwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Tunaziomba taasisi hizi ziwachukulie hatua wale wote waliohusika katika mchakato mzima wa uchaguzi mkuu, kwa umoja wetu, tutaendelea kupigania haki kwa uchaguzi huru, haki na wenye heshima," Mbowe alisoma.

Akijibu maswali ya waandishi wa habari, Mbowe alisema hawako tayari kurudia uchaguzi chini ya tume hizo za uchaguzi kwa sababu zimekosa sifa za kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Mbowe alisema tatizo halikuwapo pekee kwenye siku ya kupiga kura, bali mchakato mzima kuanzia uandikishaji na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura.

Katika kukazia yaliyosomwa na Mbowe, Zitto alisema hiyo ndiyo kauli yao na wanawakata Watanzania waifuate kwa kuwa hawana uamuzi mwingine zaidi ya huo.

"Mahali tulipofikishwa, ni lazima ama tukubaliane na ukweli au uongo, kukubaliana na haki au ukandamizaji ila uamuzi ni kukubaliana na ukweli na kukataa uongo, kukubaliana na haki na kupinga ukandamizaji," alisema.

Zitto alisema hilo siyo jambo kwa ajili ya CCM au upinzani, bali ni kuhusiana na mustakabali wa Tanzania.

"Tukiendelea namna hii na kukubaliana na kilichotokea, maana yake ni kwamba tunairudisha nchi katika mfumo wa chama kimoja.

"Kama viongozi, hatukubaliani na hali hii, tupo tayari kuongoza harakati za kudai haki, kutetea demokarasia na kuilinda nchi.

"Salamu kutoka kwa Maalim Seif ndiyo hizo alizosoma Mbowe na haya ni maandamano yasiyo na kikomo ya nchi nzima, Tanzania Bara na Zanzibar," alitamba.

Katika mkutano huo, Lissu ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, alisema katiba inasema mamlaka yote ya nchi yanatokana na wananchi kwa kupitia utaratibu wa uchaguzi ulio huru, haki na ambao unaeleweka.

"Uchaguzi uliozuia wawakilishi wa vyama kushuhudia, umejaa fujo na matumizi ya nguvu na uvunjaji sheria kwa vyombo vinavyosimamia uchaguzi, hauwezi ukatoa mamlaka yoyote kutoka kwa wananchi, ninawataka wananchi wachukue mamlaka yao tena," alisema.

Akijibu swali kuhusu ushiriki wake katika hicho wanachokiita maandamano ya amani, Lissu alisema atashiriki maandamano hayo kwa kuwa hawezi kukwepa wajibu wake kwa nchi.

**POLISI DAR**

Wakati vyama hivyo vitangaza maandamano hayo, tayari Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limeshatahadharisha wananchi kuhusu suala hilo, likisema kuwa litawashughulikia.

Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwatahadharisha wananchi wa jiji hilo kuchukua tahadhari na kujiepusha na maandamano hayo.

"Tangu matokeo yalivyoanza kutangazwa jana (juzi) yameibuka makundi ya watu, mengine yakiwa ya waliokuwa wagombea wa katika uchaguzi huu, yakifanya vikao vya siri kwa ajili ya kuingilia matokeo yanayoendelea kutangazwa, kuhamasisha wafuasi a vyama vyao kufanya maandamano.

"Wengine wameshindwa huko Hai, Kilimanjaro na Arusha, lakini wamekuja hapa kana kwamba Dar es Salaam ni shamba la bibi, nimekuja hapa kutoa onyo kwa hicho wanachokipanga," alisema Kamanda Mambosasa.

Alisema kipindi cha kunadi sera zao kimeisha na sasa Jeshi la Polisi lipo kazini kutekeleza dhima ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

"Ninatoa onyo wananchi wa Dar wapuuzeni na kama kuna anayetaka kuandamana, atangulie yeye akakutane na sisi, atangulize mke wake au mume wake kwanza," alisisitiza.

## HABARI KITAIFA

# Viongozi dini, serikali waonya maandamano

**Na Waandishi Wetu**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Waadventista Wasabato Shinyanga Mjini, John Kilinda, amewataka wagombea ambao wameshindwa kwenye uchaguzi mkuu na hawakurudhika na matokeo, wapinge kisheria badala ya kuandamana.

Wakati kiongozi huyo wa dini akitoa kauli hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amevitaka vyombo vya dola kuwadhibiti wanasiasa na wafuasi wanaochochea vurugu na maandamano kwa madai ya kutoridhika na matokeo ya uchaguzi.

Kilinda alisema hayo jana wakati wa ibada ya jana kanisani hapo kuwa wanamshukuru Mungu kwa kujibu maombi yao na hatimaye uchaguzi umemalizika kwa amani.

Alisema uchaguzi umeshamalizika na washindi wamepatikana, hivyo wakiwa viongozi wa dini, hawataki kusikia kuwapo kwa viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani, kutoka kwa wagombea ambao wameshindwa.

"Uchaguzi mkuu umemalizika kwa amani, hivyo nitoe rai kwa wagombea ambao wameshindwa na hawakuridhika na matokeo, wasiingie barabarani bali wapinge matokeo hayo kisheria," alisema Mchungaji Kilinda.

Juzi, katika Jimbo la Shinyanga mjini, Mbunge Mteule Patrobas Katambi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), alinusurika kifo baada ya nyumba yao kuharibiwak uchomwa moto na watu wanaodaiwa kuwa wafuasi wa aliyekuwa mgombea mwenza wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salome Makamba.

**NDIKILO ALONGA**

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, ameagiza vyombo vya dola kuwafuatilia nyumba za ibada na kudhibiti watakaokuwa na viashiria vya uvunjifu wa amani

Ndikilo alisema jana kuwa wakati matokeo ya uchaguzi uliofanyika Octoba 28 yakiendelea kutangazwa na baada ya kutangazwa washindi, kumekuwapo taarifa kwamba baadhi ya vyama vya siasa vinapanga kufanya maandamano.

Alisema baadhi ya vyama hivyo vya siasa vimejipanga kutumia nyumba za ibada kutangaza maandamano ambayo yanahatarisha uvunjifu wa amani.

Pia alisema kuna namba ya simu iliyogundulika kutuma ujumbe kuhamasisha watu kuingia barabaranu baada ya kuchunguzwa ilibainika inatumika ikiwa Bagamoyo. "Niwaombe wananchi mwendelee na ibada kama kawaida, vyombo vya ulinzi vinaendelea kulinda amani na kuwatafuta wanaohamasisha maandamano hatua zitachukuliwa" alisema.

Ndikilo alimwagiza Kamanda Polisi Mkoa kufuatilia mtumiaji wa namba hiyo na kumchukulia hatua za kisheria.

# Polisi wakiri kumshikilia Mazrui

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar, limekiri kuwa linamshikilia Naibu Katibu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui, tangu usiku wa Oktoba 28, mwaka huu kutokana na tuhuma mbalimbali zinazomkabili.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa jana, Kamishna wa Polisi Zanzibar, Muhammed Haji Hassan, alisema kuwa Oktoba 28, mwaka huu majira ya saa sita usiku, wakati wa kuhesabu kura, walipata taarifa za kuwapo watu waliopewa mabomu ili kulipua maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

Alisema taarifa hizo zilifanyiwa kazi na zilifanikisha kukamatwa kijana mmoja (jina linahifadhiwa) akiwa na mabomu kadhaa na alipohojiwa, alidai alipewa katika Hoteli ya Mazsons ambayo mmiliki wake ni Nassor Ahmed Mazrui.

Kamishna huyo alisema kijana huyo pia alisema wapo watu wengine waliopewa ambao wanaendelea kutafutwa.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo, jeshi liliwatumia wataalamu wa mabomu kufanya upekuzi katika Hotel ya Mazsons iliyoko Vuga na katika chumba kimoja hotelini huko, walikutwa watu 33 akiwamo kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo.

Alisema kuwa watu hao walikutwa na vifaa mbalimbali zikiwamo kompyuta mpakato 34, Ipads na nyaraka ambazo zilikuwa zina baadhi ya matokeo ya uchaguzi ambayo siyo halali, simu na vitu vingine ambavyo walikuwa wanaonekana wakitumia kuingilia matokeo ya uchaguzi mkuu.

"Hii inatokana na taarifa tulizokuwa nazo mapema kwamba kuna kikundi kilichoandaliwa kuingilia matokeo ya uchaguzi," alisema Kamishna Hassan.

Alisema watuhumiwa wote hao wamekamatwa na bado wanashikiliwa na Jeshi la Polisi hadi upelelezi utakapokamilika na hatua zaidi za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

"Ndugu wananchi, tunawataka muwe watulivu wakati upelelezi unaendelea na msijiingize katika vitendo vya uhalifu na kwa yeyote atakayejaribu kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani, hatua stahiki dhidi yake zitachukuliwa," alionya.

Vilevile, Kamishna huyo alisema wamepokea taarifa za vyama vya upinzani kutaka kuandamana nchi nzima Tanzania Bara na Visiwani, hivyo jeshi la polisi litahakikisha linapambana na waandamanaji hao.

Alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama, litahakikisha linaimarisha ulinzi muda wote ili wananchi waendelee na shughuli zao zingine za kiuchumi na kijamii.




Abiria wakiteremka kutoka kwenye ndege aina ya AirBus A220-300 ya shirika la ATCL yenye uwezo wa kuchukua abiria 130, ambayo imetua kwa mara ya kwanza katika uwanja wa ndege wa Jiji la Dodoma jana, baada ya uwanja huo, kupanuliwa na serikali na kuwezesha ndege kubwa kuanza kutua. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndege kubwa yatua jijini Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NDEGE kubwa aina ya Airbus A220-300 yenye uwezo wa kubeba abiria 132, imetua kwa mara ya kwanza katika Uwanja wa ndege wa Dodoma baada kupanuliwa kwa njia ya kutua na kufikia urefu wa kilometa 2.8.

Ndege hiyo maarufu kwa jina la Ngorongoro Hapa Kazi Tu, ilitua jana jijini hapa na kupokewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, akiwa na viongozi mbalimbali na wananchi.

Akizungumza baada ya kupokea ndege hiyo, Dk. Mahenge alisema kutua kwa ndege hiyo ni mwendelezo wa jitihada za serikali za kuharakisha maendeleo kwa Watanzania na kurahisisha huduma za usafiri wa anga.

Alisema uboreshaji wa huduma za usafiri wa ndege katika Mkoa wa Dodoma umesaidia wakazi wa jiji hilo kuondokana na gharama kubwa za usafiri walizokuwa wakitumia awali.

"Uwapo wa ndege hii ninaomba niwakumbushe tulipotoka, mwaka 2017 hapa Dodoma kulikuwa na ndege ya Auric ambayo ilikuwa inachukua abiria 12 na bei yake ilikuwa ni Sh. 530,000 kwa njia moja ya kwenda Dar es Salaam lakini uwapo wa ndege iliyokuwapo(Bombardier) na hii umesaidia gharama kushuka kwa wana Dodoma.

"Rais John Magufuli anawekeza kwenye vitu ambavyo vinawaletea maendeleo ya haraka Watanzania, uwapo wa usafiri wa ndege unarahisisha safari zetu badala ya kutumia muda mwingi kwenye gari.

"Wana Dodoma kwa niaba yenu, nimshukuru sana Rais kwa sababu anawekeza kwenye miradi inayoharakisha maendeleo ya Watanzania," alisema.

Dk. Mahenge alisema Dodoma ni kitovu cha shughuli za kiuchumi na makao makuu ya nchi na kwa upatikanaji wa usafiri wa uhakika wa ndege, itapata wawekezaji na kukuza shughuli za utalii.

"Mtalii kwenda Manyara au Ruaha ni rahisi kutoka Dodoma kuliko kutoka Dar es Salam, tunamshukuru sana Rais kwa uwekezaji kwenye Jiji la Dodoma.

"Pia, serikali inajenga uwanja mkubwa Msalato na taratibu zote zimeshakamilika na utagharimu zaidi ya Dola za Marekani milioni 30, na utakuwa na njia mbili ya kuruka na kutua," alisema.

Awali, akitoa taarifa ya upanuzi wa uwanja huo, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini(Tanroads), Patrick Mfugale, alisema uwanja huo awali ulikuwa na urefu wa kilometa 2.5, lakini kwa sasa una kilometa 2.8 na hivyo kuwezesha ndege kubwa kutua.

Alisema kazi ya upanuzi wa uwanja huo ilianza Julai mwaka huu na imekamilika Oktoba 15 mwaka huu kwa gharama ya Sh. bilioni 3.06 huku Sh. bilioni 5.8 zikitumika kulipa fidia kwa wananchi waliopisha eneo la uwanja.

"Kazi imekwisha, kilichobaki ni taa za pembeni za kuwezesha ndege hii kutua hadi wakati wa usiku," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Leonard Chamuriho, alisema uwanja huo ulipanuliwa kwa awamu mbili ambapo awali uliwezesha kutua kwa ndege ya Bombardier yenye uwezo wa kubeba abiria 76.

Alisema hatua ya kupanua ili ndege yenye uwezo wa kubeba abiria 132 imetokana na kuwapo kwa ongezeko la abiria kwenye mkoa huo.

# Machinga wanavyoweka rehani maisha ya watembea kwa miguu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

## ■Kila baada ya sekunde 24, kifo kinarekodiwa

ELFU tano viatu, elfu kumi mikoba ya kinamama, elfu tatu tu kila utakaposhika..." Sauti za wajasiriamali wadogo, maarufu machinga', zinasikika eneo la Nyerere Square mjini Dodoma wakinadi bidhaa zao kwa wateja.

Ni majira ya jioni, biashara ikiwa imechangamka kwenye eneo hilo lililoko katikati ya Jiji la Dodoma. Barabara kuu ya Nyerere inapita kwenye eneo hilo ikitumiwa na madereva wa mabasi madogo ya abiria, pikipiki na bajaj.

Katika udadisi wake, Nipashe inabaini bidhaa za wajasiriamali hao zinatandazwa juu ya mitaro kupitia maji machafu na zingine pembezoni mwa barabara, maeneo ambayo ni mahususi kwa watembea kwa miguu.

Ufuatiliaji zaidi unabaini kwamba siyo eneo la Nyerere Square tu lililokumbwa na kadhia hiyo, bali maeneo mengi ya katikati ya jiji hilo jipya sasa yamegeuka soko la bidhaa za machinga.

Maeneo hayo mbali na Nyerere Square ni pamoja na Msikiti wa Nunge, maeneo yote ya Barabara za Independence Square na Uhindini na barabara zote za jiji zinazoelekea Soko la Sabasaba.

Shida kuu inayojitokeza kutokana na utaratibu huo mpya wa kufanya biashara, iko kwa watembea kwa miguu ambao njia zao zimevamiwa na machinga, hivyo kulazimika kutumia barabara za magari.

Kinachoshuhudiwa sasa jijini Dodoma nyakati za jioni, ni milio ya honi za magari na pikipiki dhidi ya watembea kwa miguu wanaohatarisha maisha yao kwa kupita kwenye barabara za vyombo hivyo vya moto kutokana na njia za watembea kwa miguu kutandazwa bidhaa za machinga.



Machinga wakiwa wametandaza bidhaa zao eneo la watembea kwa miguu Mtaa wa Toufiq jijini Dodoma.
**PICHA: AUGUSTA NJOJI**

### KIFO KILA SEKUNDE 24

Wakati hali ikiwa hivyo jijini Ddooma, Ripoti ya Shirika la Afya Dunia (WHO) kuhusu Usalama Barabarani ya Mwaka 2018, inabainisha kuwa watu milioni 1.35 hufariki dunia kila mwaka kutokana na ajali barabarani.

Takwimu hizo za WHO zinamaanisha kwamba kila siku kuna vifo vya watu 3,699, sawa na vifo 154 kila saa na kifo cha mtu mmoja kila baada ya sekunde 24.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa nusu ya vifo hivyo vya ajali za barabarani huwapata watembea kwa miguu na ajali za pikipiki.

Kwa mujibu wa shirika hilo, idadi kubwa ya watu wanaopoteza maisha katika ajali hizo inatoka nchi za kipato cha chini kulinganishwa na nchi zenye kipato cha juu.

Chanzo cha vifo hivyo kinatajwa kuwa ni uzembe wa madereva na watembea kwa miguu pamoja na kukosekana kwa maeneo mahususi kwa watembea kwa miguu na waendesha baiskeli.

Katika uchunguzi wake, Nipashe imebaini kwamba licha ya baadhi ya barabara jijini Dodoma kujengwa zikiwa na njia maalum za watembea kwa miguu, njia hizo hazitumiwi na walengwa, badala yake machinga wanazitumia kupanga bidhaa zao.

Kutokana na hali hiyo watembea kwa miguu jijini wanalazimika kutumia barabara za magari, hivyo kuhatarisha maisha yao hasa ikizingatiwa kwa sasa kuna ongezeko la magari na watu kufuatia serikali kuhamishia shughuli zake Dodoma.

### KAULI ZA WANANCHI

Alex Mathias, mkazi wa Chang'ombe jijini, anasema mara kadhaa amenusurika kugongwa na gari kutokana eneo alilopaswa kupita katika Barabara ya Sabasaba kutandazwa bidhaa za wafanyabiashara, hivyo kulazimika kutembea kwenye barabara ya magari.

Mathias anaona kwamba ipo haja kwa uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kusimamia matumizi ya barabara kwa watembea kwa miguu ili kuepuka ajali za barabarani dhidi ya kundi hilo.

Cecilia Pius, mkazi mwingine wa jiji hilo, anashauri uongozi wa jiji kuwajibika katika hilo kwa kuhakikisha hutenga maeneo maalum ambayo machinga watapanga bidhaa zao badala ya kuguezia soko njia za watembea kwa miguu.

### USHUHUDA WA MADEREVA

Zynabu Masoudi, dereva wa basi dogo la abiria jijini, anasema uzoefu wake wa miaka 12 katika kazi hiyo unampa jawabu la sababu kuu ya vifo vingi vya ajali za barabarani iko kwa watumiaji wenyewe wa barabara.

"Kwa mfano, umeingia Barabara ya Nyerere, pale Nyerere Square, kwanza unalazimika kwenda mwendo mdogo lakini pia honi haziishi maana pembeni wanakotakiwa kupita watembea kwa miguu, kumepangwa bidhaa, watembea kwa miguu wanaingia kwenye barabara za magari, Hapo tayari kunakuwa na shida," analalama.

Dereva huyo pia anashauri barabara za watembea kwa miguu kutambuliwa na kuwe na katazo kwa wafanyabiashara kuweka bidhaa zao kwenye maeneo hayo ili kudhibiti vifo vitokanavyo na ajali za barabarani.

"Ninafikiri Jiji watunge sheria ndogo ili kulinda barabara za watembea kwa miguu, hizi ni muhimu maana maeneo hayo pia wengine wanatumia kufanya mazoezi ili kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza," anashauri.

### 'TATIZO NI VITAMBULISHO'

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyabiashara wa Soko la Sabasaba, Emmanuel Mtenga, anasema baadhi ya wafanyabishara wamekuwa wakitandaza bidhaa zao kwenye maeneo yasiyo rasmi kwa kisingizio cha kuwa na vitambulisho vya ujasiriamali vinavyotolewa na serikali.

Anasema watahakikisha wanatoa elimu kuhusu usalama barabarani na kuwahamasisha wafanyabishara kuheshimu maeneo yasiyo rasmi kwa shughuli zao za biashara.

"Ni kweli baadhi yetu tuna vitambulisho lakini tunavitumia kinyume cha kanuni na sheria zilizopo ndani ya Halmashauri ya Jiji, wengine wanafanya biashara kwenye maeneo hatarishi," anabainisha.

Victor Sijila, mfanyabiashara wa Sabasaba jijini, anasema kuwa na vitambulisho vya machinga kusiwe sababu ya kukiuka sheria na kanuni zilizowekwa na halmashauri kwa kufanya biashara holela bila mpangilio.

"Kuna wafanyabiashara wamepanga bidhaa zao kwenye maeneo hatarishi na hakuna sababu ya kukaidi kuondolewa kwenye maeneo haya ambayo siyo rasmi kwao kufanyia biashara," anasema.

### OFISA MASOKO

Nipashe inatua mezani kwa Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, kupata ufafanuzi wa mustakabali wa tatizo na kupatiwa majibu kwamba tayari kuna operesheni ya kuwaondoa machinga waliovamia maeneo ya watembea kwa miguu jijini.

Yuna anatoa onyo kwa wafanyabiashara hao kutotumia vitambulisho vya ujasiriamali vilivyotolewa na Rais John Magufuli, kukiuka sheria na taratibu za Halmashauri ya Jiji kwa kufanya biashara maeneo yasiyo rasmi.

Anasema vitambulisho hivyo vimetolewa ili kufanya shughuli zao bila kubugudhiwa na siyo kuvunja sheria na kanuni zilizopo.

"Ni kweli kuna wafanyabiashara wadogo ambao wana vitambulisho lakini wamekuwa wakiuka taratibu kwa kuvamia na kufanya biashara maeneo wanayokatazwa wakati wanatambua taratibu za jiji.

"Watembea kwa miguu wanashindwa kupita kwenye barabara zao kwa uhuru kutokana na bidhaa kupangwa kando ya barabara na imekuwa kero," Yuna anakiri.

Ofisa Masoko huyo anabainisha kuwa tayari Halmashauri ya Jiji hilo imeanza operesheni ya kuwaondoa wafanyabishara hao kwenye maeneo yasiyo rasmi ikiwamo kwenye barabara za jiji hilo kwa kuwa ni maeneo hatari kwa usalama wao na watumiaji wengine wa barabara.

Katika kufuatilia suala hilo, Yuna anazuru eneo la Nyerere Square jijini na kubaini wafanyabiashara kukiuka taratibu za ufanyaji biashara kwenye eneo hilo.

Anawataka wafanyabiashara kuacha kupanga bidhaa zao kabla ya muda uliopangwa kwenye barabara ya Nyerere Square ili kutozuia watumiaji wengine wa barabara.

Kwenye eneo hilo, uongozi wa jiji unaruhusu wafanyabiashara wadogo kupanga bidhaa zao kuanzia saa 10:00 jioni.

Hata hivyo, Yuna anasema wamebaini utaratibu huo hauzingatiwi, badala yake machinga wamekuwa wakipanga bidhaa zao kuanzia majira ya asubuhi na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara.

"Wafanyabiashara wanapaswa kufuata sheria, kanuni na maagizo yaliyoelekezwa na jiji ya kufanya biashara kwa muda waliopangiwa ili barabara hii itumike kwa shughuli nyingine," anaagiza.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, kuzungumzia suala hilo lakini kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alikataa kulitolea ufafanuzi.

HABARI KITAIFA

## CWT yapongeza ushindi wa JPM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Dodoma, Clement Mahemba, amesema wanampongeza Rais John Magufuli, kwa ushindi aliupata na kutetea nafasi yake katika uchaguzi mkuu wa 2020.

Mahemba alisema jana kuwa kwa niaba ya walimu mkoa wa Dodoma, CWT inampongeza Rais Magufuli kwa ushindi wake wa kishindo katika uchaguzi mkuu uliofanyika Jumatano wiki hii.

Alisema walimu wa Mkoa wa Dodoma wamefurahishwa na ushindi huo kwa kuwa walikuwa mstari wa mbele kumpambania ili apate nafasi hiyo katika awamu ya pili.

"Walimu tunampongeza Rais Magufuli kwa kushinda uchaguzi huu katika nafasi ya urais na tunaimani naye kubwa sana kuwa atafanya yale ambayo yalikuwa ametuahidi," alisema.

Alisema kutokana na mambo aliyowafanyia walimu katika utawala wake kwenye muhula wa kwanza wa uongozi wake, wanaamini katika miaka mingine mitano atakamilisha mahitaji yote ya walimu nchini.

"Tumempatia nafasi nyingine ili amalizie mazuri ambayo alikuwa ametufanyia katika miaka mitano iliyopita na katika kipindi hiki cha awamu ya pili, tunaamini kuwa atatufanyia mambo makubwa sana," alisema Mahemba

Aidha, alisema wakati wa kampeni Rais Magufuli aliahidi kupandisha mishahara hivyo wanaamini kuwa atatimiza ahadi yake na kuwafanya walimu watembee kifua mbele.

"Aliahidi kuwa atapandisha mishahara, hivyo tunayo imani kuwa hatujakosea na tutakuwa sehemu ya kuunga mkono serikali hii ya awamu ya tano katika kuleta maendeleo ya taifa letu,"alisema.

Pia lisema CWT inaviomba vyama vingine vya siasa kukubali matokeo yaliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kiongozi huyo wa CWT aliwataka Watanzania kuacha kudanganyika na wanasaiasa ambao wamekuwa wakishawishi watu kuingia barabarani ili kufanya vurugu kwa madai ya kupinga matokeo.

"Watanzania hatuna nchi nyingine zaidi ya hii, hivyo hakuna sababu ya kuhamasika na maneno ya wanasiasa kuingia barabarani kufanya vurugu. Lazima tuendele kuilinda amani yetu ili watoto waingie madarasani na walimu kuendelea kufundisha kwa utulivu na amani,"alisema.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, alisema Rais Magufuli ameshinda kwa kupata kura 12,516,252 kati ya kura halali 14, 830,195 zilizopigwa.

Nafasi ya pili imeshikwa na Tundu Lissu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambaye amepata kura 1,933,271.

# Jafo ampa maagizo mazito Katibu Mkuu TAMISEMI

**Na Julieth Mkireri**

WAZIRI Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Nyamhanga, kutoa maelekezo kwa waganga wakuu wa mikoa kuwapa ushirikiano wanafunzi wa taaluma ya udaktari wanaokwenda kupata mafunzo kwa vitendo.

Jafo alitoa agizo hilo juzi wakati akiweka jiwe la msingi katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha City, Tawi la Chanika.

Alitoa agizo hilo baada ya kupokea maelezo ya vikwazo vinavyowakabili wanafunzi wa chuo hicho wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo kutoka kwa uongozi wa chuo hicho.

Waziri Jafo alimtaka Katibu Mkuu Nyamhanga kuhakikisha anatoa maelekezo hayo mapema ili wanafunzi wanapokwenda kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye hospitali na vituo vya afya, wapewe ushirikiano na usimamizi wa kutosha.

"Hawa wanafunzi wanatakiwa kupewa ushirikiano kwenye maeneo wanayokwenda ili hata wanapopata ajira wawe wamekamilika kwa nadharia na vitendo," alisema.

Aidha, alisema atafanyia kazi suala gharama wanazotozwa wanafunzi wanapokwenda kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye hospitali na vituo vya afya.

"Nitafuatilia kuanzia sasa zisipofutwa basi zisiwe mzigo ili kila mwanafunzi amudu kulipia na kupata mafunzo kwa vitendo kwa wakati. Katika hili pia maelekezo yatafika kwenye Hospitali," alisema.

Katika risala iliyosomwa na Mkuu wa Chuo cha City, Fei Diwani, alisema tawi hilo lilianzishwa Septemba, mwaka huu, ikiwa ni moja ya mikakati ya chuo kuongeza udahili wa wanafunzi na kuwapa fursa Watanzania wengi.

Alisema tawi hilo jipya litatoa mafunzo ya fani za utabibu na ufamasia kwa ngazi ya stashahada .

Mkuu huyo wa chuo alisema vikwazo wanavyokabiliana navyo kuwa ni pamoja na baadhi ya vituo vya afya kutowaruhusu watumishi wake kufundisha wanafunzi wawapo katika vituo vyao wakati wa mafunzo kwa vitendo licha ya kuwa na mkataba na kufanya malipo.

Diwani alibainisha kikwazo kingine kuwa ni gharama za mafunzo kwa vitendo katika hospitali za serikali kuwa kubwa ambapo mwanafunzi anatakiwa kuchangia Sh. 50,000.

Mkurugenzi wa Mafunzo, Utafiti na Ushauri wa chuo hicho, Shabani Mwanga, aliomba serikali kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya afya.



Mwendesha guta akiwa amelisheheni mzigo unaomfanya ashindwe kuona magari yanayokuja nyuma katika Barabara ya Lumumba, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwana FA apata kigugumizi kisa ushindi

**Na Steven William,** MUHEZA

MBUNGE Mteule wa Muheza. Hamisi Mwinjuma, maarufu kama Mwana FA, ameshikwa na kigugumizi na kushindwa kuzungumza mbele ya waandishi wa habari kutokana na furaha baada ya kutangazwa kuwa mshindi.

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Muheza, Nasibu Mbaga, alimtangaza Mwana FA kuwa ndiye mshindi wa ubunge kwa kupata kura 47,578 na kumwacha mpinzani wake Yosepher Komba wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), aliyepata kura 12,036.

Mwana FA alishindwa kujieleza kwa muda mrefu kutokana na furaha ya ushindi mnono aliyoupata.

"Jamani sijui niseme nini maana nina furaha kubwa sana kwa ushindi niliopata. Nawashukuru sana wananchi wa Muheza kwa kunichagua kuwa mbunge wenu. Tutashirikiana katika kuleta mendeleo ya Muheza," alisema baada ya kukabidhiwa cheti cha ushindi.

Kutokana na mgombea huyo kutangazwa kuwa mshindi umati wa melfu ya wananchi ambao walikuwa wanamsubiri, walianza kulipuka kwa vifijo katika eneo la ofisi za halmashauri huku wakiimba na kupiga ngoma pamoja na muziki uliokuwa katika gari.

Baada ya hapo, msafara wa mbunge huyo mteule ambaye ni mwanamuziki wa kizazi kipya, ulitoka katika ofisi za halmashauri huku Mwana FA akitembea kwa miguu na kusindikizwa na umati wa watu kwenda ofisi za CCM Wilaya ya Muheza.

Msafara wa mbunge mteule huyo ulipita stendi kuu ya mabasi ya Muheza mjini, Mashine Nyingi na CCM KISHA AMTICO, Msikiti wa Ijumaa, Soko Kuu, Darajani, Manchester, Kilimanjaro Hotel, Majengo Shimoni, Mdote, Shauri Moyo, TRM, Kibanda, Semngano, Kwakopwe na hatimaye kijiji cha Kwamhanya ambako anaishi Mwana FA.

Akiwa katika ofisi za CCM Wilaya, alisema anawashukuru wananchi wa Muheza kwa kushirikiana katika kampeni na kwamba hana cha kuwapa isipokuwa atawaletea maendeleo kama walivyomtuma kwenda bungeni.

Pia aliomba ushirikiano kutoka kwake na wananchi wa Muheza atakapotekeleza ahadi zake na wasisite kumwambia kero zao kwa kuwa asingekuwa mbunge bila wao kumpa kura za kishindo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Muheza, Mohamed Moyo, alisema wananchi wa wilaya hiyo wamefanya uzalendo mkubwa kwa kumchagua Mwana FA na kwamba sasa wasubiri kuletewa maendeleo.

Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Muheza, Laick Gugu, Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya, Imani Mtumbi na Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya, Sufiani Mwedi, waliwashukuru wananchi kwa ushirikiano kuhakikisha CCM inashinda.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania wasikubali kuburuzwa kwa maslahi

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), juzi ilimtangaza mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, kuwa mshindi wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu baada ya kuwabwaga wagombea wengine 17 waliokuwa wakiwania nafasi hiyo.

Sambamba na Dk. Magufuli ambaye ametetea nafasi hiyo na kupata ridhaa ya kuongoza miaka mingine mitano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Alhamisi wiki hii, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), ilimtangaza Dk. Hussein Mwinyi kuwa Rais mteule wa Zanzibar.

Rais Magufuli, katika matokeo hayo, alipata kura 12,516,252 sawa na asilimia 84.4 ya kura zote halali zilizopigwa huku mpinzani wake wa karibu, Tundu Lissu, wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akipata kura 1,933,271 ambazo ni asilimia 13.04.

Kutokana na matokeo hayo, Rais Magufuli amevunja rekodi ya ushindi alioupata mwaka 2015. Katika uchaguzi huo, alipata kura 8,882,935 (asilimia 58.46) na kumbwaga aliyekuwa mgombea wa CHADEMA, Edward Lowassa aliyepata kura 6,072,848 sawa na asilimia 39.97 ya kura halali.

Dk. Mwinyi kwa upande wake, amevunja rekodi tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi na uchaguzi wa ushindani kwa kupata kura 380,402 sawa na asilimia 76.27 huku mwanasiasa nguli visiwani humo, Maalim Seif Sharif Hamad, akiambulia kura 99,103 ambazo ni asilimia 19.87.

Matokeo ya uchaguzi huo kwa Tanzania na Zanzibar, yameonyesha kuwa wanachama wa vyama vyote, walitumia haki yao ya kidemokrasia kuchagua viongozi wanaowataka ili wawaongoze kwa kipindi kingine cha miaka mitano kabla ya kufanyika upigaji kura mwingine.

Pamoja na matokeo hayo, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya vyama vilivyoshiriki uchaguzi huo vikidai kuwa haukuwa huru na wa haki na kwamba wameshindwa isivyo halali.

Kutokana na madai hayo, kumekuwa na vikao vya mara kwa mara kutoka baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa ikiwamo kushawishi wanachama na wafuasi wao kuingia barabarani kupinga matokeo hayo pamoja na kutaka ziundwe tume huru za uchaguzi.


Jana, kwa mfano, viongozi wa CHADEMA na ACT-Wazalendo pamoja na wagombea wao wa nafasi za urais, walifanya kikao ambacho kilitoka na maazimio ya kuwataka wanachama na wafuasi kuandamana kushinikiza kuwa matokeo yaliyotolewa si ya kweli na kutaka jumuiya ya kimataifa na za kikanda kuingilia kati.

Inawezekana madai yaliyotolewa yakawa yana chembechembe za ukweli lakini ni muhimu wanasiasa wakafahamu kwamba asiyekubali kushindwa si mshindani. Kwa mantiki hiyo, wakubali kwamba yaliyopita si ndwele wagange yajayo kwa mustakabali wa taifa.

Aidha, kama hawataki kukubali na kuendelea kutotambua matokeo hayo, ni vyema wakafuata taratibu za kisheria, kama walivyoshauriwa na baadhi ya watazamaji wa uchaguzi. Njia pekee ni kufungua kesi mahakamani kama wana sababu za kweli za kufanya hivyo.

Ni rai yetu kwa Watanzania kwamba uchaguzi umemalizika, hivyo kinachotakiwa ni kulinda amani, umoja na mshikamano badala ya kukubali kushawishiwa na kuandamana. Amani iliyopo ikitoweka ni vigumu kuirejesha. Funzo hili tunapaswa kulipata kutoka katika baadhi ya mataifa ya jirani ambayo wanajaribu kurejesha amani bila mafanikio huku maelfu ya watu wao wakiwa wamepoteza maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Majanga ya asili hayaepukiki bali muhimu kuwa na hadhari

Na Sabato Kasika

MAFURIKO ya mvua ni miongoni mwa majanga ya asili ambayo yamekuwa yakiikumba baadhi ya mikoa nchini na kusababisha madhara yakiwamo watu kupata athari za kiafya, kupoteza mali na hata maisha.

Dar es Salaam ni miongoni mwa mikoa ambayo hukumbwa na janga hilo hasa maeneo ambayo hayajapimwa, na kusababisha watu hukimbia kutokana na nyumba zao kujaa maji na kwenda kujihifadhi kwingine hadi hali inapotulia.

Zinaponyesha mvua kubwa, wakati mwingine baadhi ya barabara ikiwamo ya Morogoro eneo la Jangwani, hujaa maji na kusababisha magari kushindwa kupita, hivyo kuletwa mitumbwi ya dharura kuvusha watu.

Wakati hali hiyo ikijitokeza, tayari huwa ziko tahadhari za muda mrefu hasa za kuwahimiza watu kuhama mabondeni na kwenda kwingine, kutokana na ukweli kwamba siyo mahali salama pa kuishi.

Wako ambao walishaitikia tahadhari hiyo na kuhama na wengine bado wameendelea kuishi maeneo hatarishi na kila zinaponyesha mvua kubwa, nyumba zao hujaa maji yenye taka mbalimbali vikiwamo vinyesi vya binadamu.

Katika hali hiyo, ni wazi kwamba afya zao zinakuwa haziko salama, kwa hiyo ingawa majanga mengine hayaepukiki, kuchukua tahadhari ni suala la muhimu ili kulinda afya badala ya kung'ang'ania kwenye hatari.

Nikumbushe tu kwamba, utabiri wa hali ya hewa ni mojawapo wa nyenzo muhimu zinazoweza kuokoa maisha na pia kuepusha madhara makubwa yatokanayo na uharibifu wa miundombinu baada ya mvua na mafuriko.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imekuwa ikijitahidi kutoa tahadhari kwa watu wanaoishi maeneo ambayo si salama, lakini unaweza kusikia baadhi yao wakidai kwamba, kama ni mafuriko yatapita na wataendelea kuishi.

Hata wiki hii wakati mvua zikiendelea kunyesha, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto nayo imeingilia kati kutoa tahadhari kwa wananchi kuzingatia kanuni za afya kutokana na mvua hizo.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, kuna uwezekano wa kuibua magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kuhara damu na yanayoenezwa na mbu kama vile malaria na dengue, iwapo tahadhari hazitachukuliwa.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, anazitaja baadhi ya kanuni hizo zinazotakiwa kuchukuliwa na wananchi kuwa ni kuchemsha maji ya kunywa, kuepuka kula chakula kilichopoa, au kuandaliwa katika mazingira yasiyo safi na salama.

Kanuni zingine ni kutumia ipasavyo, vyoo na kunawa mikono kwa maji safi na tiririka na sabuni kabla ya kula, baada ya kutoka chooni, baada ya kumnawisha mtoto aliyejisaidia na baada ya kumhudumia mgonjwa.

Aidha, anawataka wananchi kutotapisha vyoo, ambalo limekuwa ni la kawaida kwa baadhi ya watu, na pia kujikinga kuumwa na mbu na kutumia vyandarua, kusimamia usafi katika mifumo ya majisafi, majitaka na mitaro.

Majanga ya asili kama mvua inaweza kuleta madhara ambayo wakati mwingine yako juu ya uwezo wa watu na mengine yapo ndani ya uwezo wao kama watazingatia maelekezo ya wataalam.

Kwa mfano suala la kuchemsha maji ya kunywa, kunawa mkono baada ya kutoka chooni na pia kutotapishwa vyoo, liko ndani ya uwezo wa kila mmoja kinachotakiwa ni kuchukua hatua tu.

Lakini bahati mbaya wapo baadhi ya watu ambao wanaona ni kama jambo la kawaida kutonawa kwa sababu ama kuchemsha maji ya kunywa, na matokeo yake mvua zinaponyesha, wanakuwa katika hatari ya kukumbwa na maradhi.

Hatari hiyo haiko kwao tu bali wanahatarisha afya za wengine, hasa wale wanaotiririsha majitaka mitaani wakati mvua zinaponyesha, hivyo ni muhimu kutambua kuwa majanga hayaepukiki, lakini tahadhari ni muhimu.

Ikumbukwe kuwa mafuriko yanapotokea husomba kila kitu yakiwamo majitakata ambayo ni hatari kwa afya za watu, hivyo ni vyema kila mmoja kuchukua tahadhari kadri inavyowezekana.

Jambo la msingi katika yote ni kila mmoja kuchukua tahadhari kulingana na maelekezo ya wataalam, kwani lengo ni kuokoa maisha, kwa kuwa majanga huwa hayana hodi na ni hatari kwa binadamu na viumbe vingine.


## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Kisa cha wanasiasa na mamantilie



Nkwazi Mhango, Canada




WANAOJUA historia ya wanasiasa kugeukana, hawatashangaa maneno ya hivi karibuni ya mwanasiasa mmoja kusema atampigia kura mgombea wa chama kingine na kumtosa mgombea waliyempitisha kwenye chama chao.

Kimsingi, ameonyesha kile ambacho Waingereza huita verisimilitude; picha ya kweli na halisi. Hii imenikumbusha kisa cha rafiki yangu.

Alikwenda kwa mamantilie kupata mlo. Akiwa anangoja mlo, alisikia mamantilie akimtuma msaidizi wake kwenda kumnunulia chakula hotelini. Jamaa alishtuka kunani; akaamua kuondoka bila kuaga wala kungoja chakula.

Maana yake nini? Mamanitilie alijua madawa machafu na sumu alivyokuwa akitumia kuvutia biashara.

Katika sakata hili kadhalika, kwa wanaojua ajenda binafsi na ithibati ya wahusika yaani ulaji, hawatashangaa wala kushuku maneno na msimamo aliouchukua mwanasiasa huyo.

Ajabu ya maajabu hata mwanasiasa mwingine (Mwenyekiti wa chama) ameamua kuukoleza kwa kukuza mgawanyiko akimuunga mkono mwenyeji wake asijue nani atafuata! Je, kinachojifunua hapa ni nini, mwisho wa mwanzo wa ndoa ya wanasiasa hao umeanza au ndo siasa? Je nani anatamchuuza mwenzake? Who's hoodwinking whom? Waingereza huuliza.

Kwa uzoefu wa uharibifu, mwanasiasa huyo ana kila sababu ya kuchekelea. Hata hivyo, itategemea.

Baada ya kuvurunda kwenye chama chake asijue aishie kwa upanga hufa kwa upanga, aweza vurunda hata huko ugenini na mwishowe akarejea "nyumbani."

Mwanasiasa wa aina hiyo hatakuwa wa kwanza wala mwisho.

Kimsingi, anachokifanya mwanasiasa huyo, amerudufu alichowahi kukifanya mwanasiasa mwingine baada ya kunyimwa kugombea urais nyumbani, japo hakwenda moja kwa moja. Alidhani angeweza kulipiza kisasi na kufikia malengo yake akiwa ndani. Yake ilikuwa: "Tutabanana humu humu."

Haikuwezekana wala hakufanikiwa. Kwa kiasi kikubwa, alifanikiwa kukiadhibu chama chake alichokihama kwa kupata kura nyingi na kupata turufu ya kurejerea nyumbani.

Tofauti na kipindi hiki, wanasiasa wanaotaka kulipiza kisasi, hawataweza, ni vigumu. Wanachofanya wanasiasa hawa, japo ni haki yao ya kidemokrasia, mipango yao itakuwa vigumu kufanikiwa. Sitaki niwahukumu japo wanahukumika kirahisi, uwezekano wa kufikia na kufanya alichofanya mwenzao ni haba.

Kama ilivyokuwa kwa wanasiasa wengine, huyu naye atajiondoa baada ya wahusika kumtumia.

Kama utabiri wetu utakamilika na wahusika kugeukana na kutumiana, ndizo siasa za kisasa na kisasi. Habari ndiyo hiyo.

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania tukumbatiane maisha yaendelee



Na Joseph Kulangwa

MICHEZO miwili ninayoipenda sana maishani mwangu ni soka na masumbwi. Usiniulize kwa nini, kwa sababu ukiniuliza sitakupa jibu nyoofu. Nitakwambia naipenda tu kwa sababu naipenda.

Lakini kwa kifupi inanifurahisha, kwa sababu ni michezo ya ushindani inayohusisha timu mbili au watu wawili wanaochuana, chini ya mwamuzi au waamuzi.

Kwa kweli kuangalia soka na kuangalia masumbwi kunavutia na kuhamasisha. Kunaburudisha na kustarehesha, hasa pale mashabiki nao wanapokuwa wamejigawa sehemu mbili, kila upande ukishangilia uupendao.

Hutokea mara zingine mashabiki kucharuka na kukabana mashati na hata kutoana ngeu na damu. Kisa ni mihemko ya michezo yenyewe, hasa pale michuano inapokuwa imekamata na mshindi hatabiriki.

Kazi huwa pevu kwa waamuzi kuamua nani ni nani, hapo ndipo pia mashabiki hucharuka na kutaka kuingia akilini mwa waamuzi, ili kuamua wanachokitaka wao. Mshikemshike hutawala viwanjani na ulingoni.

Washindani kwa maana ya wachezji nao ulingoni na uwanjani, hubuni mbinu zao chafu na safi, haram na halal, kuhakikisha kwamba wanashinda. Watumiao miguu katika soka hudiriki hata kutumia mikono. Wa masumbwi nao hutumia mbinu za kupiga chini ya mkanda, ilimradi wanacheza rafu washinde kama mwamuzi asipoona basi hushukuru Mungu wao. Nani hakumbuki Mike Tyson alivyomng'ata sikio Evander Holyfield.

Kote huko ni kutafuta ushindi kwa kila aina ya mbinu, hivyo waamuzi hutakiwa kuwa na macho angavu na makini, kuhakikisha kuwa ushindi haupatikani kwa njia haramu.

Bahati nzuri pembeni huwa kuna majaji, wakiangalia nini kinaendelea ulingoni na hutoa alama kulingana na wanachokiona na kukiamini; pembeni mwa viwanja vya soka, pia huwapo makamisaa na waamuzi wa akiba nao kuangalia nini kinajiri uwanjani. Wote hao wanapokuwa makini, ndio hufikia uamuzi wa haki na huru na kutoa ushindi wa haki kwa mhusika au wahusika. Hapo ndipo mashabiki hata kama hawaridhiki, hulazimika kukubali ili maisha yaendelee.

Lakini jambo la msingi ambalo hujibainisha katika mashindano yote hayo, ni wachezaji wawe wa soka au ndondi kukumbatiana, baada ya mchezo na kuyaacha yote hapo uwanjani, hata kama wanatoka wakivuja jasho na damu.

Ndiyo maana hata kesho yake hawataacha kusabahiana wakikutana, hata kama mmoja kavimba uso au kavunjika mguu. Huamini kwamba mchezo ni mchezo na maisha lazima yaendelee.

Kwa msingi huo, hata uchaguzi wowote ule uwe wa kisiasa au kimichezo, mimi huuchukulia kuwa sawa na mchezo tu. Huamini kwamba washiriki wa uchaguzi hususan wagombea, maadam wanatoka katika jamii moja, Watanzania, hawana sababu ya kuchukiana kwa kuwa tu itikadi ni tofauti. Kwanza wote huwa na nia moja ya kuongoza wenzao, na ndiyo sababu huomba ridhaa ya kupigiwa kura. Huchuana kwa sera na maneno mbalimbali lakini pia zikiwamo rafu za maneno ya kuudhi na wakati mwingine kutukana ingawa si staha.

Katika kampeni tunasikia kauli za huyu hafai kwa sababu hii na ile. Huyu aliahidi uongo, na hivyo akashindwa kutekeleza hili na lile. Mwingine ataahidi hiki na kile, kwamba akichaguliwa atafanya hili na lile.

Hutokewa nyakati kauli za rafu zikatumika, sawa na matumizi ya mkono kwenye soka na ngumi za chini ya mkanda kwenye masumbwi. Lakini Tume za uchaguzi huwa makini kuhakikisha kuwa rafu hizo hazikithiri. Ndiyo sababu adhabu ndogondogo hutolewa.

Lakini baada ya hapo, uchaguzi hufanyika chini ya NEC na matokeo hutolewa kwa mshindi kutangazwa, huku mshindwa akigugumia. Lakini huo ndio hubaki kuwa mchezo wa siasa.

Haipingiki kuwa baadhi ya majaji ulingoni na makamisaa au waamuzi wa akiba, hujikuta wakibagaza nafasi zao na kuchafua usimamizi wao. Bila shaka hata baadhi ya tume za uchaguzi, hujikuta katika lindi hilo na kusababisha manung'uniko.

Hata hivyo, kinachotakiwa ni kutenda haki na baada ya matokeo kutangazwa, mshindwa kuyakubali na kumkumbatia mshindi wakisubiri kuanza maisha mapya baada ya uchaguzi. Nadhani Watanzania wako hivyo au...? Alamsiki!

## KONA YA UKWELI

# Bunge lijalo lifuate nyayo Bunge la tisa



Na Thobias Mwanakatwe

UCHAGUZI Mkuu wa 2020 umeshakamilika na tayari wananchi wameshawachagua viongozi wao ambao wanaamini watawaletea maendeleo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kutokana na matokeo ambayo yamekwishatangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika nafasi za ubunge na udiwani, ni wazi kuwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kitakuwa na wabunge wengi katika jipya litakalozinduliwa hivi karibuni.

Ni katika muktadha huo, baadhi ya wananchi wameanza kuhoji je, Bunge la 12 kuwa na wabunge wengi kutoka chama tawala litakuwa na tija kama lilivyokuwa Bunge la tisa?

Kwanini bunge la tisa linaendelea kukumbukwa. Bunge la tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakumbukwa kwa mambo makubwa matatu.

Kwanza, lilikifanya chombo hicho cha juu cha uamuzi cha taifa kuwa jukwaa la mijadala yote muhimu ya kitaifa bila uoga na kufikia uamuzi mzito ulioweka misingi imara ya maendeleo ya taifa letu.

Pili, bunge hilo lilitanguliza utaifa mbele na kuibua hoja nyingi zilizowaunganisha chama tawala na vyama vya upinzani, na tatu liliboresha mazingira ya utendaji kazi wa bunge.

Itakumbuka Bunge la tisa liliongozwa na mwanasiasa mkongwe aliyejinasibu kuendesha masuala ya bunge kwa Kasi na Viwango naye si mwingine bali ni Samuel Sitta (sasa marehemu).

Kama nilivyodokeza hapo awali, ni Bunge la tisa liliibua pengine uamuzi wa muhimu katika historia ya bunge letu kiasi cha kusababisha Waziri Mkuu kujiuzulu, mawaziri wawili kujiuzulu na watendaji mbalimbali wa serikali kuchukuliwa hatua za kinidhamu na hatimaye baraza la mawaziri kuvunjwa.

Hatua hiyo ilifikiwa kutokana na uchunguzi uliofanywa na bunge kuhusu uhalali wa mkataba wa kufua umeme kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kampuni ya Richmond ya nchini Marekani.

Bunge liligundua kwamba kampuni hiyo haikuwa na usajili Marekani kama kampuni ya ukandarasi, pili mkataba wake ulikuwa wa kinyonyaji kupindukia kwani mbali na malipo ya kila mwezi ya ufuaji umeme, ilikuwa inalipwa zaidi ya Sh. milioni 160 kwa mwezi eti kufidia gharama za uwekezaji.

Katika Bunge hilo, wabunge waliolibebea bango walikuwa wabunge wa upinzani na chama tawala na kuifanya heshima ya bunge kuwa juu. Pia waliifanya taasisi moja ya kisomi ya Uingereza kuliita Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba ni bunge lenye meno.

Ni katika bunge hilo la tisa, mijadala mingine mikubwa ilifanyika na kuleta manufaa kwa taifa, mfano pesa zilizofichwa nje na baadhi ya watu.

Pia ni katika bunge hilo hilo kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kikaanzishwa ili kuimarisha uwajibikaji wa serikali katika bunge.

Hivyo basi, wakati tunaingia Bunge la 12 ambalo imedhihilisha litakuwa na wabunge wengi kutoka CCM, ni rahisi Bunge kukosa mvuto na sifa ya kuwa jukwaa la masuala muhimu kujadiliana kwa uwazi.

Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kwa Bunge lijalo kujikumbusha mara kwa mara uwajibikaji wake wa kikatiba na hivyo kufuafa nyayo za Bunge la tisa ambalo lilijizolea heshima ndani na nje ya nchi.

Nawatakia utendaji mwema uliotukuka wabunge wote waliochaguliwa na wakumbuke kutekeleza ahadi walizozitoa kwa wapiga kura wao wakati wa kampeni.

**Kwa maoni na ushauri tuwasiliane kwa email; mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Kutenga muda wa kazi na familia chachu ya ufanisi



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka
0744000066

WATU ni rasilimali muhimu mahali pa kazi. Bila rasilimali watu, hakuna taasisi, shirika wala kampuni. Kwa mantiki hiyo mafanikio yoyote mahali pa kazi yanategemea watu.

Ufahamu, utendaji kazi mzuri na furaha ya mfanyakazi ni chachu ya mafanikio mahali pa kazi.

Kwa hiyo, waajiri makini, huwekeza katika ufahamu, huwajengea uwezo wafanyakazi na watumishi wao na kujitahidi kuhakikisha wana furaha mahali pa kazi.

Kwa kutambua ukweli huo, mafunzo kuhusu wafanyakazi katika masuala mbalimbali kama vile mafunzo ya ndoa, familia na uhusiano maeneo ya kazi.

Mpango huu ni mkombozi kwa waajiri na waajiriwa.

Wafanyakazi wakiwa na matatizo ya kiuhusiano kazini na nyumbani, hali hii kwa sehemu kubwa huathiri kiwango cha furaha na utendaji wao wa kazi.

Matatizo ya ndoa na uhusiano huleta msongo wa mawazo, hali inayomwathiri mfanyakazi kisaikolojia, kiafya, kimwenendo na ufanisi katika utendaji wa kazi na hatimaye kusababisha hasara mahali pa kazi.

Kwa msingi huu, waajiri wafahamu kuwa, si wakati wote kushuka kwa kiwango cha utendaji kazi wa mtumishi au mfanyakazi mahali pa kazi husababishwa na uwezo mdogo au kukosa ufahamu.

Matatizo ya kiuhusiano au kifamilia huchangia sana katika kushusha utendaji kazi wa mtu.

Ndoa ni kiini cha familia, jamii na taifa. Hivyo, ndoa zikiwa imara, tutakuwa na familia, jamii na taifa imara.

Ndoa imara huleta tija mahali pa kazi. Kazi na familia hutegemeana.

Kazini kukiwa vizuri, kuna uwezekano mkubwa nyumbani kukawa vizuri pia. Nyumbani kukiwa na amani, kutaongeza ufanisi wa utendaji kazi mahali pa kazi, kwani baraka katika kazi huanzia nyumbani.

Kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa wa kujua kuweka mizani sawa (balancing) kati ya kazi na familia, kwani nguvu kubwa ikielekezwa katika kazi kiasi cha kusahau familia ni tatizo.

Hali kadhalika, nguvu kubwa ikielekezwa katika familia na kusahau majukumu ya kikazi, hili nalo ni tatizo.

Kikwazo wanachokutana nacho wafanyakazi wengi ni namna ya ku-balance majukumu ya kazi na familia.

Wako wafanyakazi ambao kazi zimewafanya wakose muda na familia. Akiwa kazini ni kazi. Akiwa nyumbani anaendelea na kazi za ofisini, hivyo familia haipati nafasi ya kufurahia uwapo wa baba au mama. Pia mume au mke anakosa kufurahia uwapo wa mwenzi wake.

Hali hii imesababisha uhusiano mwingine usio rasmi kuzaliwa na watoto wengi kupoteza mvuto na upendo na wazazi wao na kazi wanazozifanya.

Baadhi ya watoto wamerithi kutoka kwa wazazi wao hali ya kutokujali familia na watu wengine.

Ifahamike kuwa, kutunza familia ni zaidi ya kutoa mahitaji ya nyumbani. Kuna baadhi ya wazazi hasa wanaume, wakisha kuleta mahitaji ya nyumbani wanaona wamemaliza. Ukaribu wa mzazi kwa familia yake ni muhimu sana kwani vitu haviwezi kutoa miongozo na kujenga familia bora.

Wanandoa wasipokuwa karibu, hupunguza kiwango cha mshikamano, upendo na joto la ndoa miongoni mwao.

Hali hii pia huleta changamoto kwa watoto kwani kuna mambo ya msingi wanayakosa kutoka kwa baba au mama.

Ustawi wa familia unayumba na mahali pengine kubomoka kabisa. Mungu hakutupa kazi ili kuleta upweke katika familia, bali furaha.

Tunahitaji muda wa kazi na muda wa familia. Haitatusaidia sana kuonekana wafanyakazi bora kazini, lakini nyumbani kumeharibika. Wakati wote tukumbuke kuwa, kazi zinatuhitaji lakini familia inatuhitaji pia.

Kazi tunazofanya ni muhimu, na familia uliyopewa na Mungu ni muhimu pia.

Familia inahitaji kazi, na kazi inahitaji familia. Ni muhimu kujifunza namna ya ku-balance haya mambo mawili ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

Maisha ni zaidi ya kazi. Pamoja na kazi tunazofanya, tunahitaji muda wa kupumzika, tunahitaji muda kwa ajili ya mambo ya kijamii, tunahitaji muda kwa ajili ya wake na waume zetu, watoto wetu na tunahitaji muda kwa ajili ya masuala binafsi. Kazi hazina mwisho na haitatokea siku zikaisha.

Zaidi sana zinaongezeka siku hata siku.

**Itaendelea Jumapili ijayo.**

■ **Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa na malezi. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz**


# MAISHA

NOVEMBA 1, 2020

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili

## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Jinsi ya kukabiliana na nyufa kwenye nyumba inayoita



## KABABU ZA NYAMA

Ukurasa 14



# RAHA NA KARAHA

# Kuwa mwanamke mrembo

Ukurasa 14

# Umuhimu wa mzazi kusimamia mtoto kusoma

**Na Moses Ismail**

INAKARIBIA miaka hamsini sasa tangu uliposoma vitabu vya 'Kusoma' vya darasa la pili na la tatu katika miaka ya 1970 ulipokuwa katika madarasa hayo. Lakini hadi leo, mwaka 2020, bado unakumbuka vizuri hadithi zote za 'Juma na Roza', 'Damasi na Lusi', 'Manenge na Mandawa', 'Bora mimi sikusema' na nyingine nyingi tu.
Halafu hata kabla ya kufika darasa la nne, unakumbuka kuwa tayari ulishaanza kuosma vitabu vya 'Lugha Yetu', na ndio maana hujasahau hadithi za 'Sikiri na Sadiki, 'Kibanga ampiga mkoni', 'Sizitaki mbichi hizi' na hadithi nyingine nyingi za vitabu hivyo
Achana na kumbukumbu zako za mwaka '47, rejea katika wakati huu tulipo ambao pengine una watoto wakubwa walimaliza darasa la saba miaka ya 1990 au miaka hii 2000, umewahi kufikiria ni vitabu gani walivyosoma wao kwa wakati wao na wanakumbuka nini juu ya vitabu hivyo?
Mimi nimewahi na majibu niliyojibu yalionyesha hakuna kitabu chochote wanachokumbuka watoto wetu zaidi ya kukumbuka katuni mbalimbali na hii yaweza kuthibitisha kuwa utamaduni wa watoto wetu kusoma vutabu, umekufa.
Hili la kufa kwa utaratibu wa watoto kutopenda kusoma vitabu au hata majarida, lina athari mbaya kwa mfumo mzima wa ufahamu wao hasa kwa kujenga picha za hisia kiakili.
Mfano, unaposoma kitabu, unapata muda wa kujenga hisia mbali mbali, kwa mfano unajenga picha ya wahusika na mandhari na hata umakini wa tukio lenyewe, hapa unasaidia akili yako kutanuka".
Chukulia hadithi ya kitabu inayozungumzia nyoka mwenye vichwa saba, hii inashughulisha akili ya msomaji kumfikiria nyoka huyo wa vichwa saba namna alivyo na kujenga picha yake mwenyewe na kupata aina ya nyoka huyo.
Kinyume na kuangalia sinema au katuni, kwa kuangalia katuni na sinema msomaji hapata nafasi ya kujenga taswira yake kwa sababu tayari watengeneza sinema wameshamchagulia nyoka wao. Unamuona, hushugulishi akili tena.
Selina Gonza, ofisa mshauri wa ustawi wa jamii katika taasisi moja binafsi jijini Dar es Salaam inayoshughulika na masuala ya ustawi wa watoto na elimu anaeleza athari za kutosoma vitabu hasa nchini Marekani ambapo juhudi za makusudi zinafanywa kuwarudisha watu kwenye utamaduni wa kusoma vutabu. Anasema:
"Marekani wamegundua rai wao wengi wanatatizo la ufumbuzi wa mambo kwa sababu ya kukosa muda wa kusoma vitabu na wameshaanza kuweka mikakati ya kuhamasisha watu kupenda kusoama vitabu.
Inawezekana kuwa jamii yetu haijafikia huko kwa sababu televisheni zetu bado zinaonyesha vipindi kadhaa vya elimu ingawa vile vya burudani ni vingi zaidi, lakini wingi wa sinema majumbani mwetu unaweza kutupelekea huko.
Ni vyema basi wazazi kuwapangia watoto muda wa kusoma vitabu vya hadithi na elimu ili kuwanasua na 'mtego' huu wa kuangalia sana sinema na tamthilia kwa kuzingatia kuwa haziwajengi sana kiakili kama kusoma vitabu.

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

# QUIZ

### LE QUIZ DU WEEK

1. Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel
Présent
Je ……………
Tu ……………
Il/elle ……………
Nous ……………
Vous ……………
Ils/ells ……………

Passé
J' ………………………
Tu ………………………
Il/elle ………………………
Nous ………………………
Vous ………………………
Ils/elles ………………………

2. Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
- Présent =
- Passé = ……………

3. Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.

- Présent = ……………
- Passé = ……………
……………

4. Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
- Présent = ……………
……………
……………

- Passé = ……………
……………
……………

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA

Le quiz du week – end
- Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel
Présent
Je serais
Tu serais
Il/elle serait
Nous serions
Vous seriez
Ils/ells seraient

Passé
J' aurais été
Tu aurais été
Il/elle aurait été
Nous aurions été
Vous auriez été
Ils/elles auraient été

- Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
  - Présent = être
  - Passé = avoir été

- Weka kitenzi "Être" katika Par ticipe présent na passé.


  - Présent = étant
  - Passé = été
  ayant été

- Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
  - Présent = sois
  soyons
  soyez


  - Passé = aie été
  ayons été
  ayez été

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



Ziwa Tanganyika inapakana na mikoa mingapi ya Tanzania/

**JAMAA mmoja ameamua kunywa pombe baada ya kukutana na kituko hiki!**
**Jamaa huyo alikwenda Kariakoo kununua bidhaa, alipofika katika duka moja la kuuza majenereta alimkuta mlevi akicheza huku akikatika vilivyo.**
**Alipomuuliza anacheza nini? Yule jamaa akasema muziki unatoka kwenye jenereta ni mzuri kuliko ule wa klabuni.**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Baba anapomuua mke, kisa watoto wampatia kichapo 'nyumba ndogo'!

KARIBU tena msomaji wangu tujadili mambo mbalimbali yanayojiri katika familia zetu. Mizozo kwenye ndoa imekuwa ikishika kasi sana katika miaka ya hivi karibuni. Ni eneo ambalo yafaa kulitizama kwa makini sana.

Mizozo au migogoro hii imekuwa haileti afya kwani wakati mwingine imesababisha majeruhi, vilema vya maisha na hata vifo. Mifano ni mingi hata kupitia vyombo vya habari.

Dada mmoja hivi majuzi akanisimulia yaliyomkuta kaka yake kwa baba mkubwa ambaye alimuua mkewe kwa kipigo baada ya watoto kwenda kupiga mke mdogo (mchepuko). Baba huyu alikuwa haijali familia yake ndipo watoto walipodadisi wakagundua yupo mchepuko anayesababisha.

Dada huyu akasema kuwa huyo kaka yake ambaye hivi sasa ni marehemu, alioa mke wa ndoa na kubahatika kupata watoto wawili wa kiume. Wakawasomesha wote wakafikia sekondari.

Mara nyingi baba alikuwa akizozana na mama yao, hata kwa jambo dogo tu.

Hali hiyo haikuwapendeza watoto hao wala kumpa raha mama yao. Katika kudadisi kumbe baba alikuwa na mchepuko.

Ndio maana alikuwa akiondoka nyumbani harudi, wakati mwingine hata baada ya siku mbili. Na kila aliporudi lazima alizusha ugomvi na kumpiga mkewe.

Watoto hao ambao mmoja alikuwa kidado cha kwanza na mwingine kidato cha nne, walichunguza hadi wakajua alipokuwa akiishi mke huyo mdogo wa baba yao. Wakavizia siku baba aliposafiri, wakaenda kumvamia mama huyo na kumpiga kisha kuharibu vitu mbalimbali ikiwamo TV na kadhalika, wakaondoka.

Baba aliporudi na kukuta tukio hilo, akamrudia mkewe na kuanza kumpiga akihisi kwamba huenda mama ndiye aliyewatuma watoto kwenda kumvamia mchepuko wake.

Watoto wakamtetea mama yao wakati akipigwa wakashindwa. Baba akawakana wale watoto kwamba siyo wa kwake.

Mama akawa amejeruhiwa vibaya wakaitwa majirani kumsaidia na kumkimbiza hospitalini.

Baadaye waliitwa ndugu za mke kumhudumia wakati wa matibabu. Mama huyo aliuguzwa kwa takriban miezi mitatu lakini ikashindikana akafariki dunia.

Inasemekana aliumizwa sana hasa sehemu za kichwani hata kumpotezea kauli.

Ndugu za mume nao waliposikia tukio hilo la ndugu yao kumpiga mkewe hata kusababisha kifo chake, wakamkana kwamba siyo ndugu yao na wala akipatwa na tatizo lolote asiwashirikishe apambane na hali yake. Ndugu za mke nao wakatoa msimamo kwamba marehemu atazikwa kwao na siyo kwa mumewe.

Jamaa baada ya mazishi ya mkewe akaamua kumhamishia mchepuko wake pale nyumbani alipokuwa akiishi na familia yake. Watoto walipokuja juu akawafukuza na kuwaambia hawatambui. Ndipo wakaondoka kwenda kuishi kwa ndugu za baba yao.

Maisha yakaendelea akazaa na yule mwanamke watoto wawili, mmoja wa kiume mwingine wa kike. Baada ya miaka minne ya kuishi pamoja, jamaa akaugua sana hadi huyo mama akazidiwa kumhudumia. Ndugu wa mume wakawa kimya kwani walishamkana kwa kusababisha kifo cha mkewe. Hatimaye naye akafariki.

Mpenzi msomaji, bila shaka umeguswa na ukatili huu wa kijinsia ambao umepigiwa sana kelele na jumuiya ya kimataifa. Jitihada mbalimbali zimefanyika kujaribu kuzuia lakini bado matukio ni mengi katika familia nyingi.

Ukiona tatizo haliondoki au linajirudia rudia, fahamu kuwa ipo nguvu nyuma yake. Zipo roho ambazo hutesa sana ndoa katika familia zetu, zikiwamo roho za mafarakano na mitala.

Roho ya mafarakano ni moja ya silaha anayotumia shetani kuhakikisha familia zinasambaratika. Leo uhusiano mzuri ndani ya familia umekufa kwa sababu ya mafarakano. Mizozo isiyoisha kati ya wanandoa, hivyo kutishia amani, utulivu unaotakiwa.

Mitala ni roho nyingine ambao pia inawezekana ndiyo ilikuwa inamtesa baba aliyesababisha kifo cha mkewe kwa kipigo. Hii ni silaha nyingine anayotumia ibilisi kuvuruga ndoa nyingi. Hii ni roho inayochipua ndoa za wake wengi, kuolewa au kuoa na kuachika au kuachwa.

Hizi roho huwa hazionekani mwanzoni mwa mahusiano, bali husubiri ndoa inapofikia kwenye mafanikio makubwa hasa ya kiuchumi, ndipo huibuka na kuvuruga. Lazima tutafute sana nguvu ya Mungu ili kutuepusha mikosi na balaa katika maisha yetu.

**Je, una maoni au kisa ungependa tujadili pamoja? Tuma ujumbe mfupi kupitia namba namba 0715268581. Namba hii ipo pia WhatsAPP. Tukutane wiki ijayo.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Pre-Form One ni kitanzi kwa wazazi, serikali iliangalie hili

KILA mzazi hupenda kuona mwanawe anasoma shule nzuri ambayo kipimo cha kwanza ni mazingira ya kujifunza na kujisomea pamoja na shule inavyofaulisha wanafunzi wengi kwenye mitihani ya kitaifa.

Kutokana na uhitaji huo, shule binafsi zimekuwa kimbilio kwa kuwa inaaminika ndiko wanafunzi hufaulu kwa kiwango cha juu na mazingira yake ni mazuri. Huo ndio ukweli.

Wazazi hushindana kupeleka watoto katika shule hizo za kibiashara kwa lengo la kutaka wapate kilicho bora zaidi na hatimaye kuwa miongoni mwa watoto waliosomeshwa vizuri.

Aidha, wazazi wamejikuta katika mazingira magumu ikiwamo shule hizo kuwa na kiwango kikubwa cha ada ambazo wakati mwingine hufikia milioni sita kwa mwaka mmoja kwa mwanafunzi wa darasa la kwanza hadi la saba.

Ukifuatilia kwa kina fedha hizo hugawanywa katika usafiri, maendeleo ya shule, sare za shule ambazo ni lazima mzazi anunue katika shule husika kwa bei iliyowekwa na shule, karatasi na mahitaji mengine. Katika kuonyesha hawatozi ada kubwa basi ada huwa ndogo na ili mwanafunzi asome katika shule husika, ni lazima alipe fedha yote na unapohoji sababu kubwa ni kodi kubwa inayotozwa na serikali na gharama za uendeshaji wa shule huku wakitaka kupata faida.

Katika namna ya kujipatia fedha shule hizo zimeweka utaratibu wa mwanafunzi kufanya mtihani wa kujiunga ambao hulipiwa kati ya Sh. 10, 000 na 100,000 na hakuna uhakika wa kupata shule husika, hivyo mzazi analazimika kumpeleka mwanaye kwenye shule zaidi ya moja.

Pia shule hizo zimeanzisha utaratibu wa mwaka mmoja kusoma 'Pre-form one' ambayo baadhi ya shule ni lazima kusoma kwa miezi minne hadi mitano na kwa kuwa mzazi anatakiwa kulipa ada.

Wakati mwingine katika mtihani wa kujiunga na shule husika unakuta wanajua kabisa uwezo wao ni wanafunzi 120 lakini hufanya usaili kwa wanafunzi 4,000 au zaidi na kila mmoja anatakiwa kulipia Sh. 30,000 ambayo kwa wanafunzi wote wanatengeneza Sh. milioni 120.

Cha kushangaza baada ya siku mbili matokeo yanatolewa kwa waliofahulu kiasi cha kuzua maswali mengi kama; hawa walisahihisha saa ngapi? na je, kulikuwa na umakini katika usahihishaji?

Na mbaya zaidi baada ya usahili ni lazima apitie Pre-form One vinginevyo bado hajakamilisha sifa za kujiunga na shule husika.

Cha kujiuliza mitaala imetengenezwa kwa ajili ya kukamilishwa ndani ya mwaka mmoja yaani Januari hadi Desemba, sasa huu muda wa kabla ni wa nini? Kwa mwanafunzi ambaye kasoma katika shule binafsi na amepikwa vizuri?

Shule husika kati ya wanafunzi 4,000 imechuja na kupata 120 ambao ni bora zaidi ya wengine. Sasa hiyo Pre-Form One ya nini tena? Na ada ya nini tena? kama wangekuwa wamechukuliwa waliofeli ingeeleweka kwamba wanasaidiwa ili waweze kulingana na wenzao.

Matokeo yake watoto wanashindwa kupumua kwa kuwa baada ya kumaliza darasa la saba amepelekwa kusoma tena na muda mfupi anaanza masomo ya mfumo rasmi wa serikali.

Mzazi analipa ada ya Preform One alafu analipa ada ya Form One tena, huu ni mzigo mzito sana hata kama mzazi ndiye aliyetaka kusomesha mtoto wake shule nzuri.

Ifike mahali serikali iingilie kati, maana biashara inazidi kushika atamu bila kuwaonea huruma wazazi, ambao wanajinyima ili watoto wao wapate elimu.

Natambua kuwa shule hizo zinafanya biashara na wanapaswa kupata faida ili kukabiliana na kodi na madai mengine ya serikali ikiwamo gharama za uendshaji, lakini ni muhimu sana wakajali wazazi.

Haipendezi na haikubaliki 'kuwachuna' wazazi kwa kisingizio cha elimu yao, badala yake iwe ni kufuata utaratibu ambao hata Wizara ya Elimu itaubariki kwamba ndiyo unapaswa kufuatwa.

Mathalani, kipindi cha Corona shule zilifungwa na watoto walikaa nyumbani kwa miezi mitatu lakini baadhi ya shule zilitoza fedha ya usafiri na chakula ambacho watoto hawakula, na shule hizo hizo zilikuwa hazilipi mishahara wafanyakazi wake kwa madai ya kuathiriwa na Corona, lakini mzazi asipolipa fedha hizo mwanaye anafukuzwa shule.

Kama haitoshi zipo shule zilijitengenezea muhula wake na kupata muhula wa siku 30 badala ya miezi mitatu, yaani kuanzia Novemba mosi hadi Disemba 4, ni muhula mpya na mzazi anapaswa kulipa ada kamili vinginevyo abaki na mwanaye nyumbani.


Haya ni maumivu sana ambayo hayastahili kufumbiwa macho na Wizara ya Elimu, vinginevyo ni kuendelea kuruhusu elimu kuwa biashara na ndiyo maana wengine huiba mitihani ili kuaminisha wazazi kuwa shule husika ni nzuri kitaaluma.

**TUTAFAKARI!**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**









Bwana na bibi Erasmus Rweyemamu, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kufunga ndoa hivi karibuni, Bukoba mjini, mkoani Kagera.

# MITINDO



# SUTI ZA VITENGE

## Ruksa kwenda kokote kule

SUTI za vitemge ni aina ya mtindo wa mavazi ambao umezidi kupata sifa kwa watu mbalimbali ambao wanaopenda kwenda Kiafrika zaidi.

Nguo hizi zimepata umaarufu kutokana kupendwa na mastaa wengi wa Kiafrika, kutokana uzuri wake unaomfanya mtu kuwa na muonekano wa kupendeza.

Kwa upande mwingine, wabunifu wa mavazi wamezidisha hamu ya wateja wao, baada ya kila kukicha kuja na aina mpya ya suti ambazo zinawapagawisha wateja wao.

Faida ya kuwa na suti za vitenge zipo nyingi, lakini baadhi ni kutokuwa na wasiwasi wapi unaweza kwenda, kutokana na aina hiyo ya nguo kukubalika katika sehemu nyingi ikiwamo ofisini, kumbu za starehe, mikutano na matembezi ya jioni.

Tazama picha tofauti ujionee jinsi suti za vitenge zinavyombadilisha mtu na kuonekana maridadi zaidi.

# UREMBO

# RAHA NA KARAHA kuwa mwanamke mrembo



KILA mwanamke aliyeumbwa na Mungu ana sifa ya kuwa mrembo, lakini kuna baadhi urembo wao umezidi na kuwafanya kuwatofautisha na wengine.

Wapo Wanawake walioumbwa vizuri kuanzia sura, shingo, kifua, kiuno hadi miguu.

Pale anapopita kila mtu humtizama na kukiri kwamba Mungu ameumba, hapo ndipo hiutwa mwanamke huyo ni mrembo kupindukia.

Hata hivyo, mwanamke mwenye urembo wa kupindukia ana wakati mgumu kukabiliana na mazingira yake na watu wanaomzunguka.

Mara nyingi anakabiliwa na upweke, kutokana na watu kumuona kama mtu wa kipekee kiasi ambacho inakuwa vigumu kuwa karibu naye.

Kutokana na hofu hiyo, idadi kubwa ya warembo hao wanashindwa kuolewa au kuishi na wapenzi katika muda sahihi na kusababisha wengi wao wanajikuta wakiishi peke yao.

Je, ni kwanini hali hiyo huwatokea wanawake warembo wa kupindukia? Hizi ni sababu zinazowafanya watu kuogopwa.

**MAJIVUNO**

Wanawake wenye uzuri wa kupindukia kwa kawaida hujiamini kupita kiasi, huwa na kiburi pamoja na majivuno.

Kama hawatakuwa na watu wa kumrudisha kwenye msitari, mwishowe huwa na tabia ya kupenda starehe na matumizi ya gharama ya juu.

Wanaume wengi hawapendezwi na tabia hizi na inakuwa vigumu kumfikia kwa hofu ya kushindwa kudumu naye.

**MARINGO**

Wanawake wazuri sana huwa na maringo yanayokinaisha, anapotembea au kufanya jambo lolote anataka kuonekana.

Tabia hiyo inasababisha watu kumuona kama anajiona na mwenye kuringa.

**UBINAFSI**

Mara nyingi wanawake wa aina hii wanakuwa na tabia ya ubinafsi wakiamini kila kizuri duniani ni chao.

Wanachoamini hawawezi kukataliwa na wanaume na wakati mwingine huwa na dharau.

**HAWAPENDI KUZAA**

Wanawake warembo huwa na mashaka kuhusu kupata watoto mapema, wakihofia kuharibu uzuri wao.

Wanaamini mwanamke akizaa huchoka mapema, ngozi husinyaa haraka jambo ambalo huaribu muonekano wao.

# MAPISHI

## Na Mary Geofrey

# KABABU ZA NYAMA



**Mahitaji**

MINOFU ya nyama ya ng'ombe, kuku au samaki, yai moja, kipande kimoja cha mkate, pilipili hoho moja, kitunguu maji kimoja, kitunguu saumu kimoja, karafuu iliyosagwa, chumvi na limao.

Namna ya kuandaa

Kitunguu maji na pilipili hoho, vyote vikatwe vipande vidogo, ponda kitunguu saumu kwenye kinu, halafu viweke pembeni.

Andaa nyama ya samaki, kuku au ya ng'ombe kwa kukata vipande, ioshe, kisha ichemshe na weka ndimu na chumvi.

Nyunyuzia pilipili manga, usiongeze maji kwenye nyama, acha ikauke halafu weka kitunguu.

Loweka kipande cha mkate kwenye maji, kitoe na kikamue kisha changanya na mayai yaliyopasuliwa na kukorogwa na kuchanyika vizuri.

Bandika kikaangio jikoni, weka mafuta mengi kiasi, subiri yachemke na tengeneza umbo la mviringo kutoka kwenye nyama, samaki au kuku, kisha chovya kwenye rojo la mkate na mayai.

Tumbukiza mviringo wa mchanganyiko kwenye mafuta, mmoja baada ya mwingine ili kupata matokeo mazuri kwa kutumia kijiko kikubwa chenye madundu ili kuchuja mafuta.

Mchanganyiko wako ukae kwenye mafuta kwa muda wa sekunde tano hadi nane mpaka uwe rangi ya kahawia na hapo utakuwa umeiva vizuri.

Ipua na acha vikauke na tayari msosi wako utakuwa tayari kwa kuliwa. Unaweza kula kama kifungua kichwa au wakati wowote kwa kutumia soda, juisi au maji.

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## JINSI YA KUKABILIANA NA NYUFA KWENYE NYUMBA



NYUFA kwenye nyumba ni miongoni mwa matatizo ambayo huweka doa ustawi wa nyumba hizo.

Tatizo la nyufa ni miongoni mwa magonjwa sugu yanayosumbua majengo na miundombinu mingine kwenye ujenzi, haijalishi ni jipya au la zamani.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Razack Kimbai, anasema nyufa wakati mwingine hutokea kwa namna ambayo ni vigumu kuzuilika kutokana na mazingira au muundo wa ubunifu na usanifu wa muhimili wa jengo lenyewe.

Kimbai anasema miongoni mwa sababu kuu zinazochangia kuwapo na nyufa kwenye nyumba au jengo ni kutitia na kwamba ni jambo la kawaida hasa kwa yale ambayo hayana muda mrefu baada ya kujengwa.

Anasema hali hiyo husababishwa na udhaifu wa msingi kushindwa kuhimili uzito wa jengo, kusinyaa na kutanuka kwa udongo uliobeba msingi wake, kuoza kwa baadhi ya mimea au viumbe vilivyopo chini ya ardhi, kukua au kuoza kwa mizizi ya miti na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutegemea asili ya mazingira ya eneo husika.

Anasema nyufa hutokea zaidi pale upande mmoja wa jengo unapotitia na upande mwingine kubaki katika hali yake tatizo ambalo hutokea kwa kutegemeana na ubora na umakini wa matokeo halisi ya upembuzi yakinifu wa kisanifu kabla ya ujenzi.

Kimbe anasema ni muhimu sana kufanya uchunguzi wa kisanifu kwenye eneo husika kabla hujaanza ubunifu na usanifu wa kile unachokwenda kujenga ili kuepukana na nyufa baada ya ujenzi.

Sababu nyingine ya nyufa anasema ni kutokidhi vigezo vya usanifu na ubunifu majengo.

Kwamba mabadiliko ya haraka ya teknolojia ya uhandisi yanayoendelea kutokea duniani yanawaacha nyuma baadhi ya wataalamu wa ujenzi, hali ya uchumi na ubora wa vitendea kazi ni vikwazo kwa baadhi ya wataalamu wa ujenzi.

Anasema ubunifu na usanifu majengo ni jambo mtambuka linalohitaji uwezo na ujuzi wa hali ya juu sana tofauti na wengi wanavyofikiri na kwamba kazi hiyo ni muongozo wa utendaji katika kila hatua wakati wa ujenzi.

Anasema kutokidhi vigezo vya ubunifu na usanifu majengo ni rahisi sana kutengeneza matatizo kwenye majengo yanayokuwa yanajengwa.


# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU ZA KUEPUKA UNYEVU KWENYE UKUTA WA NYUMBA.

1: Weka madirisha yanayoingiza hewa ya kutosha
2: Weka bomba chini kuondoa unyevunyevu.
3: Epuka kufulia ndani ya nyumba.
4: Epuka kuoga mara kwa mara kama bafu lipo ndani ya nyumba.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NILIAHIDI JUKWAANI NIKIPEWA RIDHAA NITA-KWENDA KUISHI NA WAKULIMA KIJIJINI. ...MUNGU ALIVYO WA AJABU 'WAMENIPA'
UKISIKIA MTU ANALAANIKA KWA AHADI YAKE, NDIO HII.
NIMEKEREKA SANA! MIKELELE YOTE ILE JUKWAANI LAKINI UNAAMBULIA KURA MBILI TU!
KWANZA ZILE KURA KANIPIGIA NANI NA NANI?... NATAKA NIWAJUE UKAWASUTE
NIMEPATA KURA 'MOJA TU' FIKIRIA ITAKUWA YA NANI KATI YANGU NA MKE WANGU
SIJIBU NISIJE NIKAVUNJA NDOA YAO!
NAKEMEA WAPIGA KURA MLIOKUWA NAMI KWENYE KAMPENI MKANI-KAANGA KWENYE KURA...PEPO TOKA!
UKISIKIA PLANI-BII NDIO HII
NAAMINI KAULI YA 'KUNA MAISHA BAADA YA UCHAGUZI' ONA ULIVYOKULA POZI BAADA YA KUSHINDWA,
HIVI KWA AKILI YAKO NINGESHINDA NINGEKUBALI? NINGEWAULIZA VIZURI NINA MAAJABU GANI HASA...
NAMUUNGA MKONO ALIYE-SHINDA BADALA YANGU SITAKI MAKUU.
KAMA SIO YEYE ALIYEKUWA AKIHUBIRI VURU-MAI AKISHINDWA!
KITAANI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KUBALI KAMA YESHATOKEA...

HABARI KIMATAIFA

# Tetemeko laua 27 Uturuki

**ANKARA, Uturuki**

WATU 17 wamefariki dunia baada ya tetemeko la ardhi kuupiga mji wa pwani ya Aegean, nchini Uturuki na kisiwa cha Samos cha Ugiriki, siku ya Ijumaa.

Vikosi vya waokoaji hadi sasa vimefanikiwa kuwaokowa watu wapatao 100, kufuatia tetemeko hilo la ardhi lenye ukubwa wa kipimo cha Richter cha 6.6 kupiga miji hiyo.

Mpaka jana watu 27 wamethibitika kufariki dunia na wengine 800 wamejeruhiwa.

Tetemeko hilo lililikumba eneo la bahari linalojumuisha nchi za Uturuki na Ugiriki.

Idadi hiyo ya watu waliofariki, 25 walipatikana maneneo ya pwani ya Uturuki na wengine wawili kutoka Samos.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, nyumba 20 zilibomolewa kabisa katika mji wa Izmir ndani ya nchi hiyo.

Matetemeko mingine zaidi ya 400 yalifuatia, lakini hayakuleta hathari zaidi.

Viongozi wa Uturuki na Ugiriki waliwasiliana kwa njia ya simu kuzungumzia juu ya maafa hayo.

Jumla ya mahema 750 yameshaandaliwa kuhifadhi walioathirika na janga hilo. Aidha kumefunguliwa majiko ya kuhamishika yenye uwezo wa kulisha zaidi ya watu 50,000, huku mamlaka husika zikiwatolea wito wenyeji kukaa mbali na majengo yaliyoharibiwa.

Wakati huo huo, serikali ilitangaza kuzifunga shule zote kwa muda wa wiki moja kama sehemu ya hatua za kiusalama.

Waziri wa Elimu, Ziya Selcuk, aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter, kwamba katika muda huo uchunguzi utafanyika katika shule zote kuangalia athari zilizopatikana.

Izmir ni mji wa tatu kwa ukubwa nchini Uturuki, wenye idadi ya wakazi wapatao milioni 4.3.

Kijiografia Uturuki ni nchi iliyoko kwenye eneo lenye hatari ya kutokea matetemeko ya ardhi mara kwa mara.

**DW**



Askari wa uhamiaji wa Marekani, akitoa maelekezo kwa wahamiaji wanaovuka mpaka kupitia daraja linalotenganisha mji wa Nuevo Laredo, Mexico, kwa ajili ya kuwatenganisha watoto wao na kuwahifadhi katika nyumba maalum. **(PICHA: AP)**

# Armenia, Azerbaijan zashutumiana

**GENEVA, Uswisi**

NCHI za Armenia na Azerbaijan, zimelaumiana kwa mara nyingine baada ya mashambulizi ya mabomu kulenga makazi ya raia.

Mapigano hayo yamevunja makubaliano yao ya awali ya kutowashambulia raia.

Mashambulizi hayo yaliripotiwa kutokea saa kadhaa baada ya kufikiwa makubaliano ya kumaliza mgogoro huo, katika mazungumzo yaliyofanyika mjini Geneva nchini Uswisi

Mazungumzo hayo yalijumuisha mawaziri wa mambo ya nje wa nchi hizo mbili na wajumbe kutoka Ufaransa, Urusi na Marekani.

**DW**

# Trump, Biden kampeni za lala salama

**WASHINGTON, Marekani**

WAGOMBEA wa nafasi ya urais nchini Marekani, Donald Trump na Joe Biden, wameingia hatua ya lala salama za kampeni zao za kuomba kura kabla uchaguzi utakaofanyika keshokutwa.

Rais Trump, anayepeperusha bendera ya chama cha Republican na Biden kutoka chama cha Democratic, kila mmoja anatumia mbinu mbalimbali kuwashawishi wapiga kura kumchagua katika nafasi hiyo.

Katika hatua ya kuongeza nguvu, Rais mstaafu Barack Obama, ataungana na Biden, kufanya kampeni kwenye jimbo la Michigan wakati Donald Trump anayetetea nafasi yake, atakuwa katika jimbo la Pennsylivania ambalo ni muhimu katika uchaguzi huo.

Mgombea mwenza wa Biden, Kamala Harris, aliendeleza kampeni zake katika jimbo la Texas kuanzia juzi ili kujaribu kuligeuza jimbo hilo liwe la chama cha Demokratic kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1976 wakati wa Rais Jimmy Carter.

Endapo chama cha Demokratic kitashinda kwenye jimbo hilo, itakuwa pigo kwa Trump, ambaye analitegemea kwa ushindi wake.

**DW.**

## Ufaransa yaimarisha ulinzi baada ya mauaji

**PARIS, Ufaransa**

UFARANSA imeimarisha ulinzi katika miji mbalimbali baada ya kusambaza maelfu ya polisi kulinda usalama katika mitaa kuhofia kufanyika matukio ya kigaidi.

Hatua hiyo ilichukuliwa wakati uchunguzi ukifanyika juu ya tukio la watu watatu kuuawa na mhamiaji kutoka Tunisia, baada ya kuvamia kanisa katika mji wa Nice, kusini mwa Ufaransa.

Mtuhumiwa wa mauaji anayetambulika kwa jina la Brahim Issaou, alipigwa risasi mara kadhaa na polisi na kukimbizwa katika hospitali moja akiwa katika hali ya mahututi.

Rais waUrafansa Emmanuel Macron, aliitisha kikao cha dharura kujadili tukio hilo, kiongozi hiyo tayari ameidhinisha doria za kijeshi kwenye makanisa na kwenye sehemu nyingine kabla ya siku kuu ya watakatifu inayofanyika leo.

**DW.**

## Watu 19,000 waambukizwa corona Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**

SHIRIKA la habari la Ujerumani DPA, limeripoti zaidi ya watu 19,000 wameambukizwa virusi vya corona katika muda wa saa 24 nchini Ujerumani.

Ripoti hiyo, ilieleza kulingana na taarifa iliyotolewa na taasisi ya Robert Koch ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza, idadi hiyo ni kubwa kurekodiwa tangu kuanza kwa ugonjwa huo.

Watu zaidi ya 500,000 wameambukizwa virusi vya corona nchini Ujerumani tangu mwezi wa Desemba mwaka jana. Kati ya watu hao, 10,452 wamefariki.

Ujerumani ilitangaza hatua zaidi ya kuzuia kuenea kwa maambukizi itakayoanza kutekelezwa Jumatatu wiki ijayo.

**DW**

## Waziri Mkuu Libya kuendelea madarakani

**TRIPOLI, Libya**

WAZIRI Mkuu wa Libya, Fayez Serraj, anayeongoza serikali inayotambuliwa kimataifa, ameahirisha uamuzi wake wa kujiuzulu.

Serraj ambaye alitaka kujiuzulu mwisho wa mwezi wa Oktoba, ataendelea kubaki madarakani hadi mazungumzo ya awamu ya pili ya amani yakamilike.

Awali kiongozi huyo alitangaza kukabidhi madaraka kwa mamlaka ya utendaji mwishoni mwa mwezi huu wa Oktoba.

Msemaji wa Baraza la Juu la Uongozi Libya, Ghaleb Al-Zaqlaly, alisema matumaini yake ni kuona kamati ya mazungumzo itaweka mbali masilahi binafsi na ya kikanda, ili nchi hiyo imalize mgogoro wa sasa kwa amani na maelewano.

Libya imetumbukia katika machafuko tangu kupinduliwa kwa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Muamar Gaddafi mwaka 2011

**DW**

## MAKALA

# Umaskini ni sifa mtu kuwa kiongozi mzuri?



Na Magabilo Masambu

SUALA la uongozi limekuwa na mitazamo tofauti katika jamii. Mitazamo hii inatokana pia na historia ya maisha katika familia zetu. Wako wanaoamini kwamba kiongozi mzuri hutokea katika familia maskini na wengine wanaamini kuwa kiongozi bora hutokea katika familia tajiri.

Wote wanaweza kuwa sahihi kwa maana kwamba kila analowaza mtu kabla ya kubadilishwa wazo au fikra na mtu mwingine huwa wazo hilo linakuwa sahihi kwa utashi wake.

Tuanze na wale wenye dhana ya umaskini pengine wako sahihi au hawako sahihi. Kwa nini watu huamini basi kwamba kiongozi bora hutoka familia maskini?

Mara nyingi tumesikia viongozi wengi wakijinadi nyakati mbalimbali katika majukwaa au katika maeneo tofauti kwamba wao ni watoto wa maskini. Wengine wamejaribu hata kueleza namna gani wamehangaika kufika walipo, wakieleza maisha ya taabu waliyopitia katika makuzi yao na kwamba wamesomeshwa kwa taabu.

Watu hao wamekuwa wakieleza kuwa mpaka wamefikia hatua walizo nazo leo, wamepitia mengi na kwamba shida za watu wanazijua, hivyo wakipewa nafasi watazishughulikia vizuri kwa sababu si wageni wa matatizo hayo wameyaishi!

Dhana hii imetumika kwa miongo kadhaa na kufika mahali kutuaminisha kwamba kumbe ili uwe kiongozi lazima uwe maskini kwanza na sheria za maadili ya viongozi zikatungwa kwamba lazima tufahamu kiongozi anapoingia madarakani ana mali kiasi gani. Sijui kama kuna sheria za kuchunguza kiongozi akitoka madarakani awe na mali kiasi gani!

Lakini ni kwa kiasi gani dhana hii ina ukweli? Je, ni kweli viongozi wanaotokea katika familia maskini wamekuwa msaada kwa maskini wenzao? Au viongozi wengi wanatumia njia hii kama propaganda ya kuwapatia madaraka tu?

Wananchi pia tunafurahia na tunamfurahia sana kiongozi wa namna hii. Ni kweli matumaini yetu kwao yanatokana na hali ya umaskini tulio nao na tuna imani kwamba akitokea mtu wa namna hii anaweza kutusaidia kwa sababu anataja maisha ya wengi tuliopitia na kusema ukweli huwa wengi wanasema ukweli juu ya maisha yao? Lakini je, ni kwa kiasi gani viongozi hao hutumia historia ya maisha yao kubadilisha maisha ya wengine? Hili ndilo jambo tunalopaswa kujiuliza kila mmoja wetu.

Kinyume cha mategemeo ya wengi, imekuja kuonekana kwamba kumbe viongozi wengi wanaosema wametokea katika maisha ya ufukara, wanapopata nafasi wanakuwa kama ng'ombe mwenye kiu kubwa ya maji na kwamba sasa wamefika ziwani, hivyo lazima wanywe maji ya kutosha na ya akiba. Matokeo yake wanajikuta wameharibu moja kwa moja dhamira yao ya mwanzo iliyowapa madaraka.

Umaskini katika Afrika na hasa nchini mwetu, umetumika kama zana ya kuwapatia watu uongozi. Wako wanaosingizia hali hiyo huku wakiwa na mali nyingi. Pia wako wanaosema ukweli wa maisha yao ajabu ni kwamba wengi wao wanaingia wakiwa maskini wanatoka wakiwa matajiri wa kutupwa pamoja na kujinadi kwamba tuwachague ili watuletee maendeleo na kwamba maisha yetu wameyaishi na wanayajua.

Mataifa yaliyopiga hatua za kimaendeleo nao wana dhana yao kwamba kiongozi kwanza lazima awe aliyetosheka na mali kwa kuamini kwamba akichaguliwa hatakuwa na kiu ya kujitajirisha kutokana na fedha za umma. Wanaamini katika utajiri na imeonekana kwamba viongozi wa namna hiyo wanatamani kuona watu wanakuwa matajiri zaidi kuliko kuwafanya wawe maskini.

Nimewahi kusoma mahali fulani katika makablasha kuhusu uongozi wetu hapa Tanzania kuwa si sehemu ya kujitajirishia bali ni huduma na kwamba kiongozi yeyote lazima awe na kazi halali ya kujipatia kipato.

Nadhani dhana hiyo imegeuka siku hizi badala yake imekuwa kwamba uongozi ni sehemu ya kujitajirishia ndiyo maana pengine mwaka huu katika uchaguzi mkuu, watu wengi walijitokeza kuchukua fomu za kuwania uongozi ili wakatajirike.

Mwisho niseme kwamba kama kweli tunatokea familia duni tukipata madaraka tuwasaidie watu watoke tulikotokea kwa sababu tukifa hatutazikwa na mali tulizo nazo bali tutakuwa peke yetu.

Zaidi tutaondoka na dhambi tunazotenda dhidi ya wengine tukiwa duniani na hesabu yetu itakuwa siku ya mwisho. Mbele ya Muumba, tutahesabiwa kadri tulivyotenda na tutapewa hukumu inayotustahili.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Upinzani, vituko vya mashabiki wa bendi za Msondo na Sikinde



Na Adam Fungamwango

KUNA siku niliandika kuwa nitaelezea asili ya upinzani wa Juwata Jazz iliyokuwa na mtindo wa Msondo Ngoma na Miliman Park, maarufu kama Sikinde Ngoma ya Ukae, pamoja na vituko vya mashabiki wa bendi hizo mbili. Niligusia kidogo kuwa upinzani huo ulitokana na Sikinde kumchukua Muhidini Maalim Gurumo mwaka 1978.

Baada ya hapo, mwaka 1979, ilimchukua Hassan Rehani Bitchuka ambaye alibaki kuwa mwimbaji kiongozi tegemeo. Hapo ndipo vita kali ya maneno, kutungiana nyimbo za mafumbo na hata upinzani wa kimuziki baina yao ulianza.

Kiasili, Sikinde ilitakiwa iwe na upizani na Dar Intenational kwani ilichukua karibu wanamuziki wote kasoro Marijani Rajab ambaye wakati huo alikuwa amesimamishwa bendi na kiongozi Abel Balthazar. Ikumbukwe pia Abel alikuwa Msondo kabla ya kwenda kuanzisha Dar Intenational.

Baada ya Balthazar kutimka na wanamuziki wa Dar International kwenda kuunda Mlimani Park Orchestra, mmiliki wa bendi hiyo, alimwita Marijani na kumkabidhi vyombo.

Naye alikusanya wanamuziki wengine wapya na kuliongezea jina kundi lake na kuwa na mtindo maarufu wa 'Super Bomboka', akiwa na maana bomu lililopasuka. Hapo alikuwa akiwapiga vijembe wanamuziki waliokwenda Sikinde.

Hata hivyo, ni Msondo na Sikinde ndizo zilizoingia kwenye vita kali ya ushindani wa muziki pamoja na kuwagawa mashabiki, wengine Msondo na wengine Sikinde. Ikawa kama Simba na Yanga.

Sasa shughuli inakuja kwenye vituko vya mashabiki wa bendi hizo. Kwanza kabisa mashabiki wa pande zote mbili walikuwa wakijazana kwenye kumbi ambazo bendi hizo zinapiga.

Walikuwa wakienda popote pale jijini Dar es Salaam. Wakati mwingine walisafiri hadi mikoani kuzifuata bendi zao.

Kwenye jiji la Dar es Salaam, bendi hizo zilipiga kwenye kumbi zote maarufu, lakini kumbi ambazo ndizo kama makao makuu ya Sikinde zilikuwa DDC Kariakoo, DDC Magomeni Kondoa, DDC Keko, Mlimani Mpakani na Super Stereo Bar, Temeke.

Msondo nao kumbi zilizokuwa kama ndiyo makali makuu yao ni Amana Social Hall (Ilala), Wami Bar (Mwananyamala) na Kigongo Bar (Buguruni).

Kuna wakati Sikinde iliingia kwenye anga za Msondo, Wami Bar, lakini walifanyiwa fujo na mashabiki wa Msondo kiasi kwamba kiongozi wa bendi, Gurumo, alitangaza rasmi kuwa hawatapiga tena kwenye ukumbi huo. Na kweli ikawa hivyo. Wami Bar ilikuwa kama kambi hasa ya Msondo.

Bendi hizi zilikuwa na aina tofauti na mashabiki, wakati mwingine utawajua hata kwa mwonekano tu. Mashabiki wa Sikinde walikuwa ni watu fulani hivi kwa lugha ya watoto wa mjini wa sasa wanaitwa 'matozi' au zamani 'mabitozi.'

Ni vijana watanashati wanaojipenda na wengine wanaofanana na hivyo. Kwa mashabiki wa muziki wa sasa, wanafanana na wale wa bongo fleva. Mashabiki wa Msondo ni watoto wa mjini, watoto wa uswahilini au 'uswazi'. Ni vijana masela ambao unatashati ni msamiati mgumu kwao.

Yeyote yule atakayeamua kwenda Msondo, awe amejiandaa hasa. Ni Msondo Afya haswa. Unaweza kukutana na mtu anacheza huku akipigwa mkwara kuwa hataki hata kivuli chake kikanyagwe.

Wakati huo vyombo vilikuwa vya aina ya 'Ranger'. Zile spika kubwa zilikuwa nane mpaka 10 hivi. Zilikuwa zikifungwa kwenye kona mbalimbali za kumbi au baa. Sasa kila spika ilikuwa inazungukwa na kuchezwa na mashabiki wa sehemu fulani.

Kuna wa Mwananyamala, Kinondoni na Magomeni walikuwa na yao. Buguruni, Ilala na Misheni Kota walikuwa na yao. Temeke, Tandika na Chang'ombe walikuwa na yao. Sasa ajichangaye mtu wa Buguruni, aende kwenye spika ya watu wa Mwananyamala, anatafuta ugomvi huyo, kitakachompaka atasimulia.

Wakati bendi nyingi ukivaa visivyo huruhusiwi kuingia, ni Msondo tu ndiyo walikuwa wakiruhusu yeyote aliyevaa, au kunyoa vyovyote aingie, kutokana na asili ya mashabiki wao. Kwenye kuvaa pensi, chini buti zaidi ya lile la jeje waliingia, lakini bendi zingine marufuku.

Ukisikiliza muziki na mapigo ya Sikinde si ya kasi sana kutokana uchezaji wa mashabiki wao, lakini nyimbo nyingi za Msondo ziko kasi kutokana na mashabiki wao wengi kupenda hivyo.

Yakitokea mashindano, au mapambano baina ya bendi hizo mbili kupiga pamoja, mashabiki wa Sikinde ni lazima wawe wanyonge, wakiwaogopa wenzao wa Msondo kutokana na muonekano wao, wanavyocheza, na hata wanaipambania bendi yao.

Kuhujumiana kulikuwa ni kawaida baina ya bendi na mashabiki wenyewe. Kuna dhana inasema katikati ya miaka ya 1980, umeme ulikatika kwenye ukumbi la Friends Corner, Manzese wakati Msondo ikipiga, lakini cha ajabu kote ulikuwapo.

Mashabiki wa Msondo wakaenda kuangalia waya uliokuwa ukileta umeme kwenye ukumbi huo hadi nje kwenye mlingoti na barabarani. Wakawa waifuata waya kwa kuiangalia juu ulipokwenda na kukata kona.

Walikwenda nao hadi walipogundua umefika DDC Magomeni Kondoa ambako Sikinde ilikuwa inapiga ndipo ulipokatikia. Wakajua ni hujuma. Wakaitwa wahusika wakatengeneza na rhumba likaendelea kama kawaida Manzese.

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka, na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe Sesilia kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-6

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

ZAHIR unasikia, unanitia aibu mimi mbele ya ndugu zangu na watu wanaonizunguka."

"Kwa nini unasema hivyo Cecy."

"Haiwezekani kaka zangu wanakwenda hospitalini na wake zao, wapenzi wao kumwona mama, mpaka mdogo wangu Badaka naye anakuja na mpenzi wake, mimi nakwambia njoo na mimi nionekane wa maana wewe unakataa. Wewe utakuwa hunipendi."

"Nakupenda ila niko bize mpenzi wangu."

"Siyo kweli, jana nilionana na rafiki yako Mussa, akaniambia hujasafiri wala nini, ulikuwa hapa hapa Dar."

"Huyo Mussa ulikutana naye wapi? Au anakutaka, anaanza kuleta fitina ili akuchukue?"

"Yaani ushaniona mimi najiuza eee? Nitoke kwako, halafu nikamchukue na rafiki yako, yaani umenichoka kweli."

"Lakini mpenzi, pesa si nilikutumia shilingi laki mbili kwa ajili ya mama?"

"Wewe pesa ndiyo umeona kitu cha maana ee, mimi nakutaka wewe ufike, siyo pesa zako, umedhalilisha na umenitia aibu, nasema hivi, mimi naona tuachane tu."

Yalikuwa na mazungumzo ya kwenye simu baina ya wapenzi hao. Cecy alianza kuona makosa aliyoyafanya.

Alipata kila kitu, kasoro mapenzi ya kweli. Mapenzi ya kweli ni yale ya mwanaume kumjali mpenzi wake. Kujali hisia zake. Kuwapenda anaowapenda. Kuonekana kuguswa na matatizo yanayowapata anaowapenda na wanaomzunguka.

Zahir hakuwa hivyo. Lakini hayo alikuwa akiyapata kutoka kwa Mashaka. Kwa mbali alianza kuona makosa aliyoyafanya.

"Wewe huyo bwana anayekuzuzua huyo siku hizi, nikimpata lazima nimfanyizie."

Sauti ya Zahir ilimshtua tena kutoka kwenye mawazo.

"Umfanyizie nani. Wewe hujui mwanamke anataka nini. Wewe unadhani mwanamke anataka pesa tu. Kwenu hunipeleki. Kwetu hutaki kuja. Yaani mimi umenifanya kama mtumwa wako. Mimi siyo mtumwa wa pesa." Alisema na kukata simu. Hakutaka tena kusikia sauti ya Zahir.

Si kweli kwamba alifuta namba ya Mashaka kama alivyosema. Alipiga. Ilipita nusu dakika bila kupokelewa.

Mashaka wakati huo alikuwa anaangalia soka kwenye kibanda umiza. Kutokana na kelele za watu




**"Nzuri habari yako?" Aliitikia kwa mashaka mashaka kama jina lake akiwa hajui nini kitaendelea. "Mashaka, mimi nina mazungumzo na wewe kama utakubali. Nataka tuongee, nakuomba niruhusu."**

kushangilia hakusikia mlio.

Cecy alinyong'onyea. Machozi yalianza kumlengalenga. Alijua Mashaka hakupokea kwa makusudi baada ya maneno yake machafu aliyokuwa akimtolea siku za nyuma.

Aliamua kupiga tena. Safari hii Mashaka alisikia kwa mbali.

Alipotoa na kuangalia jina alishtuka. Na yeye pia hakufuta jina la Cecy. Hata hivyo aliogopa kupokea. Alichoogopa ni kukoga matusi. Hakujua ni kitu gani kilichomfanya apige simu muda ule. Anakumbuka siku tatu zilizopita alikuwa hospitalini kumwangalia Mama Cecy.

"Anataka kunikataza kwenda kumwangalia?" Alijiuliza. "Lakini si jana ameshatoka hospitalini?"

Tangu alipopigiwa simu na kuambiwa afute jina na wasijuane hajawahi kupigiwa simu yoyote. Na hata ile ya mama Cecy kuwa mgonjwa alipigiwa na shemeji yake Badaka.

Awali alitaka asipokee lakini kuna sauti nyingine ikamwambia apokee tu na kama ataanza kuongea maneno yake mabovu, basi atakata simu mara moja. Akapokea.

"Hujambo Mashaka?" Ilikuwa sauti ya utulivu na ya unyeyekevu. Mashaka aliijua vyema ile sauti. Ilikuwa ya Cecy. Lakini alichoshangaa ni kwamba haikuwa ya Cecy wa sasa anayemfahamu. Ni Cecy yule wa mwanzo.

"Nzuri habari yako?" Aliitikia kwa mashaka mashaka kama jina lake akiwa hajui nini kitaendelea.

"Mashaka, mimi nina mazungumzo na wewe kama utakubali. Nataka tuongee, nakuomba niruhusu."

"Uongee na mimi?" Hakuamini.

"Ndiyo Mashaka." Cecy alijibu kwa sauti ya upole.

Ni upole uliomtisha zaidi Mashaka kuliko ukali wake.

"Amepatwa na nini huyu?" Alijiuliza.

"Sawa, wapi sasa?"

"Popote pale, kama unataka tukutane sehemu, njiani, kituoni, au nyumbani kwako, wala siyo mbaya, ninachotaka mimi nikutane na wewe haraka."

"Sawa, hakuna neno. Kesho siendi kwenye mishughuliko yangu, njoo nyumbani nitakuwepo muda wote tu."

"Ahsante Nakushuru."

*************************************

Kabla ya yote. Cecy aliamua kwenda saluni kujipamba. Mtoto wa kike anapambwa na kupambika. Ilikuwa siku ambayo ameahidiana kwenda kuonana na mpenzi wake wa zamani Mashaka.

Alikuwa tayari ameshamwomba mdogo wake Badaka amsindikize. Lengo la Cecy ni kwamba bado anamuonea aibu Mashaka na woga pia kutokana na maneno makali na machafu aliyomtamkia huko nyuma, hivyo hakujua nini Mashaka anaweza kuamua.

Badaka anaweza kuwa msaada mkubwa kwake itakapobidi. Pia anatambua kuwa Badaka na Mashaka wana maelewano makubwa. Damu zao zinapatana, hivyo hakuwezi kuharibika neno.

Badaka naye hakukataa. Binafsi alimpenda mno Mashaka kuliko Zahir. Alitambua kuwa Mashaka anampenda sana dada yake, na ndiyo maana huwa anajitoa kwenye shughuli zote za kijamii zinazowahusu. Iwe sherehe, ugonjwa au msiba.

Alibeba furaha na huzuni za mpenzi wake Cecy kama za kwake. Nyakati za furaha za Cecy alifurahi pamoja naye na nyakati za huzuni alihuzunika naye bila kujali kipato kidogo alicho nacho.

Alimwangalia Zahir anamuona ni mtu mwenye uwezo wake, lakini ni mtu anayemhitaji zaidi Cecy kujifurahisha nafsi yake tu bila kujali chochote kinachomhusu.

Hata yeye mwenyewe alishawahi kumuona mara moja tu, tena akiwa na haraka kama mtu anayetaka kwenda kuzima moto.

Anakumbuka jinsi dada yake alimpomtolea povu siku ile kule kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

Anakumbuka usaliti wote ambao dada yake ameufanya, hivyo kitendo cha kuonekana kujutia, aliona ana haki ya kumsaidia dada yake arejee kwa mwanaume ameyependa na kujali.

Badaka pia aliona atatumika kwenye usuluhishi kwa sababu anaelewana sana na Mashaka. Hata siku ambayo kulitokea tafrani hospitalini, ni yeye ndiye aliyeizima na kumchukua kwenda naye. Kabla ya hapo ndiye aliyempigia simu Mashaka. Na hata mama yao alipolazwa kwa mara ya pili, alimpigia na kumtaarifu pia.

Na hata mama yao Bi. Magdalena ameshaanza kumfahamu kwa kumuona mara mbili akija hospitalini kumtazama, ingawa anadhani kuwa anaweza kuwa ni mpenzi wake na si wa Cecy. Ni kwa sababu mara zote mbili wanakuwa wote wawili.

Hayo yote alipoyafikiria alijiona ni mtu muhimu kuongozana na dada yake.

Cecy, baada ya kujipamba alivaa nguo mpya nzuri, zilizomkaa vema. Lengo ni kuushtua upya moyo wa Mashaka ambao anaona kwa sasa utakuwa amesinyaa.

Akaona haitoshi. Akapika chakula kitamu ambacho Mashaka anakipenda. Ulikuwa ni wali wa nazi, samaki aina ya kitoga. Aliunga na nazi, akiweka bamia na nyanya chungu.

Ni chakula ambacho anakipenda mno.

Alipulizia na marashi ambayo aliwahi kununuliwa naye huko nyuma. Safari ikaanza kwenda nyumbani kwa Mashaka.

INAENDELEA JUMAPILI



## 'JINI BABA' KUTAMBULISHWA RASMI

MSANII anayekuja kwa kasi wa muziki wa Bongo Fleva, Joshen Adam, maarufu kama 'Giny' amesema wimbo wake mpya 'Giny Baba' utaanza kuruka hewani wiki inayokuja.

Akizungumza na Nipashe, Giny amesema katika hatua ya kuutambulisha rasmi, atakuwa ya kutembelea vyombo vya habari kwa lengo la kuzungumza na mashabiki wake.

"Uongozi wangu umejipanga vyema kutambulisha singo yangu kwa aina ya kipekee, nitatembelea vyombo tofauti vya habari kwa nia ya kukutana na mashabiki wangu na kuusikia kwa mara ya kwanza wimbo wangu," amesema Giny.




# HAMISA MOBETO
## wapotezee wenye midomo

MWANAMUZIKI na mwanamitindo, Hamisa Mobetto, amesema hawezi kukata tamaa kutokana na maneno ya watu, badala yake anaamini kutimiza ndoto zake.

Akizungumza kwenye shoo ya Friday Night, inayorushwa na kituo cha EATV, Hamisa amesema licha ya watu kumkosoa hajui kuimba, yeye anaendelea kufanya kazi yake hiyo ambayo inampatia pesa.

"Mimi ni mtu ambaye huwa sikati tamaa, huwa naamini katika matarajio yangu mwenyewe, naamini ndoto zako ni za kwako ambazo umepewa na Mungu, kwenye haya maisha ukisikiliza watu wanachosema hutofika, kama ulipangiwa kufika sehemu fulani utafika tu hata kama iwe vipi" amesema Hamisa Mobetto.



## Ali Kiba awachambua wanamuziki wavivu

MWANAMUZIKI maarufu nchini, Ali Kiba, amewataka wasanii wa Bongo Fleva kuacha tabia ya kutoa nyimbo mfululizo bila malengo, kwani kwa kufanya hivyo wanajiua kisanii.

Kiba amesema kwa upande wake anafanya muziki kwa ajili ya kumpatia pesa, na ndio maana anapotoa nyimbo moja huchukua muda mrefu kutoa mwingine ili umrudishie gharama zake pamoja na kulinda heshima yake.

"Kuna baadhi ya wasanii nahisi muziki wanauotoa unakaa muda mfupi kutokana na kutokuwa na malengo, wanaharibu mfumo wetu wa zamani wa wimbo kukaa muda mrefu baada ya kutoa singo kila mwezi. Lazima wimbo uheshimike kwa kukaa muda mrefu kama Sinderella," amesema Kiba.

## HABARI MICHEZO



# GUARDIOLA
## ANA BAHATI KUTOFUKUZWA CITY

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa zamani wa Manchester City na Liverpool, Dietmar Hamann amesema Kocha Pep Guardiola ana bahati hajafukuzwa kazi hadi sasa.

Hamann amebainisha kwamba, City haitashinda taji la Ligi Kuu England wala Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka ya karibuni.

Mjerumani huyo amewazungumzia City baada ya kuanza vibaya msimu huu kwenye Ligi Kuu England.

City ilibeba taji la Kombe la Ligi msimu uliopita huku wakikomea robo fainali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na hawakuonyesha upinzani kabisa dhidi ya Liverpool kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu uliopita.

Licha ya City kupata mafanikio makubwa tangu Guardiola alipowasili, Hamann haamini kama watakuwa na uwezo wa kufanya timu hiyo kuwa bora na kunyakua mataji.

"Ukitazama rekodi zao kwenye Ligi ya Mabingwa huoni kama kutakuwa na kitu cha ziada," amesema akiiambia Sky Sport.

"Bila shaka alikuwa na wakati mzuri Barcelona na pengine itabaki kuwa hivyo.

"Hakufika fainali akiwa na Bayern Munich na City. Kwa kifupi tu hawapo kwenye ubora mzuri chini yao. Sipendi makocha wafukuzwe, lakini naamini kocha mwingine anaweza kuleta kitu tofauti."

# MOURINHO: MSIMAMO WA LIGI EPL SIO ISHU



**LONDON, England**

JOSE Mourinho anaamini msimamo wa Ligi Kuu England hauna maana yoyote wakati huu wa mwanzo mwa msimu licha ya Tottenham kuanza vizuri.

Tottenham wapo nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi wakipitwa ponti mbili na vinara Everton huku wakielekea kwenye mchezo wa leo Jumapili dhidi ya Brighton and Hove Albion.

Spurs imepoteza mchezo mmoja tu katika mechi saita za ligi na wamefunga mabao 16, mengi zaidi kuliko timu yoyote, na wanapewa nafasi ya kuwania taji la ligi msimu huu.

Lakini kocha wa Tottenham, Mourinho amesema ni mapema mno kutoa hukumu kuhusu msimamo wa ligi hiyo kwa sasa.

"Naamini msimamo sasa haumaanishi chochote. Naamini kwamba, Februari hadi Machi, unaweza kuangalia msimamo na kuelewa hali halisi ya mashindano," amesema.

"Sidhani kwa sasa ni jambo zuri kuzungumzia kwamba timu ipo kwenye nafasi gani, maana ni mapema mno kufanya hivyo.

"Tuna matokeo mazuri kwenye ligi, lakini hatuwezi kusema kwa sasa tuna nafasi nzuri sana kwenye Ligi Kuu England. Ni mapema mno kusema hivyo."

# Dean kuamua United dhidi ya Arsenal

**MANCHESTER, England**

MWAMUZI, Mike Dean ametajwa ndiye atakayechezesha mchezo wa leo Jumapili kati ya Manchester United dhidi ya Arsenal utakaofanyika kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Uteuzi huo haujapokelewa vyema na baadhi ya mashabiki wa timu zote mbili kubaki na wasiwasi mkubwa, kwani Dean anatajwa kuwa mtata sana.

Dean mwenye umri wa miaka 52, amechukulia umaarufu mkubwa kutokana na aina yake ya uamuzi anavyofanya anapokuwa kwenye mechi.

Amechezesha mechi nyingi kuliko mwamuzi yeyote, akichezesha mechi 513, wakati anayefuatia amechezesha mechi 415, ameonyesha kadi nyekundu 105, anayefuatia ameonyesha kadi 67 na ametoa penalti 173, anayefuatia penalti 96, akifunika kwenye vipengele vingi kuliko vya waamuzi wengine wote kwenye historia ya Ligi Kuu England.

Mashabiki wa Arsenal wameonyesha wasiwasi wao juu ya Dean na rekodi yake ya penalti ambazo amekuwa akiwapa United.

Rekodi zinaonyesha United imepewa penalti 36 kwenye michuano yote tangu ilipoanza kunolewa na Ole Gunnar Solskjaer.

Rekodi pia zinaonyesha United imeibuka na ushindi kwenye mechi 40 na kupewa penalti 18 katika mechi 74 ilizocheza mwamuzi akiwa Dean, huku Arsenal wao wakishinda mara 36 na kupewa penalti sita tu katika mechi zao 75 alizochezesha mwamuzi huyo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PIRES AMPELEKA MBAPPE MADRID

Aeleza itakuwa ni sehemu sahihi kwa mshambuliaji huyo kama anataka kuona anakua zaidi katika uchezaji...

**PARIS, UFARANSA**

KYLIAN Mbappe anatakiwa kujiunga na Real Madrid kama anataka kuendelea kukua kama mchezaji, kwa mujibu wa nyota wa zamani wa Ufaransa, Robert Pires.

Mbappe mwenye umri wa miaka 21, amekuwa akihusishwa sana na kuhamia Madrid baada ya kung'ara akiwa na Paris Saint-Germain, ambako ana mkataba hadi mwaka 2022.

Pires, ambaye alikataa kuichezea Madrid kipindi chake cha uchezaji, amesema Mbappe anatakiwa kujiunga na miamba hao wa LaLiga na nyota huyo wa zamani wa Arsenal na Ufaransa analiona hilo linawezekana kabisa.

"Bila shaka. Mimi ni Mfaransa, naipenda Paris Saint-Germain na napenda yeye kubakia kwenye Ligue 1," alisema akiiambia AS.

"Lakini kama anataka kuendelea kukua kama mchezaji, anatakiwa kusajiliwa Real Madrid."

Kocha wa Madrid, Zinedine Zidane awali alibainisha namna gani anavutiwa na Mbappe, ambaye ana mabao sita na pasi za mwisho tano katika mechi saba msimu huu.

Mbappe alitoa pasi za mwisho mbili kwa Moise Kean wakati PSG wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Istanbul Basaksehir, Jumatano iliyopita.

Tangu kuanza kwa msimu wa 2017-18, Mbappe ana pasi za mwisho nyingi zaidi (15) kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kuliko mchezaji mwingine yoyote.

Zidane pia amekuwa kwenye presha pale Madrid, ambaye ameshinda mechi moja kati ya nne zilizopita katika mashindano yote.

"Nafikiri ni watu wasiofikiria wanazungumza kuhusu zama za mwisho za Real Madrid wakati inapopoteza mechi mbili kabla ya El Clasico na sare dhidi ya Borussia Monchengladbach," amesema Pires.

"Najua kuna presha kubwa Madrid, lakini kocha na wachezaji wanahitaji kutulizwa kwa sababu kufungwa ni sehemu ya mchezo.

## KWA UFUPI

**MUSTAFI NJIA MOJA**
MLINZI wa Ujerumani, Shkodran Mustafi mwenye umri wa miaka 28, amekataa ofa ya mkataba mpya Arsenal na ameitaarifu klabu hiyo kwamba ana mpango wa kuondoka, wakati mkataba wake wa sasa utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. **(Football London)**

**LAMPARD AMTAJA RUDIGER**
KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard yuko tayari kumjumuisha, Antonio Rudiger kwenye mipango yake ya kikosi cha kwanza, kufuatia mazungumzo ya kina na mlinzi huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akihusishwa na timu za Tottenham na Paris St-Germain. **(Mail)**

**PALACE, TOWNSEND WATETA**
KLABU ya Crystal Palace imeanza mazungumzo na winga wa England, Andros Townsend mwenye umri wa miaka 29, kuhusu mkataba mpya baada ya kufanikiwa kuzima mipango ya West Brom iliyokua inamtaka katika kipindi cha majira ya joto **(Football Insider)**

**WEST WAMKERA BILIC**
KOCHA wa West Brom, Slaven Bilic amekasirishwa na mtendaji mkuu wa klabu hiyo baada ya kumruhusu mlinzi wa Misri, Ahmed Hegazi mwenye umri wa miaka 29, kuondoka na kujiunga na Al-Ittihad inayoshiriki Ligi Kuu Saudi Arabia, bila yeye kujua **(Sun)**

**ROSE, SPURS KITAELEWEKA**
KLABU ya Tottenham Hotspur ina matumaini ya kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba wa mlinzi wa kushoto ambaye ni raia wa Uingereza, Danny Rose, lakini nyota huyo mwenye miaka 30 anatarajia kutaka kulipwa zaidi ya pauni milioni 2.5 ya thamani ya mkataba wake uliobaki, ambao unamalizika June mwakani. **(Football Insider)**

**BODI EPL YAJIPANGA**
BODI ya Ligi Kuu England itaiweka kando katika juhudi zake za kuishawishi wizara ya mambo ya ndani ya nchi hiyo kuleta visa maalumu, baada ya England kujiondoa rasmi Umoja wa Ulaya. **(Mail)**

**LIVERPOOL YAMKANA KABAK**
LIVERPOOL haina mpango wa kumsajili mlinzi wa Schalke, Ozan Kabak mwenye umri wa miaka 20 ambaye ni raia wa Uturuki **(Liverpool Echo)**

**MOYES ATETEWA WEST**
WACHEZAJI wa West Ham wanamuunga mkono kocha wao, David Moyes na wanataka aongezewe mkataba mpya. **(Mail)**

**UMTITI AIKATAA ARSENAL**
MLINZI wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Samuel Umtiti ambaye ana umri wa miaka 26, amekataa mazungumzo ya kujiunga na Arsenal. **(Canal+, via Football London)**

**LASNBURY KUONDOKA VILLA**
KIUNGO wa England, Henri Lansbury ambaye ana umri wa miaka 30, amekataa ofa kutoka Aston Villa ya kumaliza mkataba wake na klabu hiyo. (The Athletic, via Birmingham Mail)

**GUARDIOLA ATOA NENO**
PEP Guardiola amesisitiza Manchester City ilifikiria kumsajili straika mpya katika kipindi cha majira ya joto, lakini haikuweza kumpata yule wanayemhitaji. **(Manchester Evening News)**

**ESSIEN AMFUNDA LAMPARD**
KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Michael Essien amemtaka Frank Lampard kutafuta mfumo mzuri pale Stamford Bridge baada ya kuwa na mwanzo mgumu msimu huu. **(Goal.com)**



HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS, U-17 ZAPAA NA MATUMAINI

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kimeondoka nchini leo na kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kushiriki mashindano ya COSAFA kikiwa na malengo ya kufanya vyema kwenye michuano hiyo.

Twiga Stars ni mwalikwa katika michuano hiyo inayotarajiwa kufanyika kuanzia keshokutwa hadi Novemba 14, mwaka huu mjini Port Elizabeth.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime alisema kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea katika mashindano hayo, na wanaamini wanakwenda kupambana na si kusindikiza.

Shime alisema mechi zote zitakuwa ngumu hasa kutokana na historia ya Twiga Stars inapokuwa kwenye michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

Kocha huyo alisema kikosi chake kinatarajia kutumia mashindano hayo kama sehemu ya maandalizi ya mechi yao ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za Vijana dhidi ya Senegal itakayofanyika baadaye mwaka huu.

"Mipango na mikakati yetu ni kuona tunafuzu kucheza fainali za dunia, tutatumia mashindano haya kujiimarisha na kuongeza uzoefu kwa wachezaji wangu, ila tutahakikisha tunaendelea kupeperusha vyema bendera ya nchi katika kila mashindano tunayoshiriki," Shime alisema.

Nahodha wa timu hiyo, Amina Bilali, aliliambia gazeti hili wanaenda kwenye michuano hiyo wa lengo la kupambana na wanafanya hivyo kwa sababu wanataka kulitangaza vizuri jina la Tanzania.

"Tuko tayari, tunaenda huko kupambana, tunajua kila mechi kwetu itakuwa ni fainali, ni mashindano mafupi, hivyo ukipoteza mechi moja, unajiweka katika nafasi ngumu ya kusonga mbele, tuombeeni tukatimize kile tunachotarajia," nahodha huyo alisema.

Wakati huo huo, kikosi cha Timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17 (U-17), kinatarajia kuondoka kesho kuelekea kwenye michuano hiyo ya COSAFA.

Kikosi hicho cha vijana kitakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Edna Lema wakati Mkuu wa msafara ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), Amina Karuma.



Bondia Twaha Kiduku (mwenye kaptula ya bluu), akishangilia baada ya kutangazwa mshindi dhidi ya Sirimongkhon Lamthuam kutoka Thailand, katika pambano la kuwania mkanda wa WBC lililofanyika kwenye Ukumbi wa PTA, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Kiduku awapa ubingwa Watanzania

**Na Saada Akida**

BONDIA Mtanzania, Twaha Rubaha maarufu Twaha Kiduku, ametaja sababu kubwa iliyomfanya akaibuka mshindi dhidi ya Mthailand Sirimongkhon Lamthuam, ni kufanikiwa kusoma vyema mbinu za mpinzani wake huo.

Kiduku aliibuka mshindi katika pambano la kuwania mkanda wa Dunia wa WBC kwenye uzito wa Super Welter lililofanyika juzi jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kiduku alisema baada ya kuangalia mapambano mbalimbali ya Mthailand huyo, alibaini aina ya uchezaji wake na kulazimika kubadilisha mbinu zake na hivyo alifanikiwa kumweka 'mtegoni'.

Kiduku alisema alilazimika kujifua zaidi baada ya kufahamu rekodi nzuri ya mpinzaki wake ambayo katika mapambano 101 aliyocheza, amepoteza manne tu.

"Nashukuru kwa kuiwakilisha vyema nchi, ushindi huu sio wangu kama Kiduku au watu wa Morogoro, ushindi huu ni wa Watanzania wote, pia kuhusu huyu jamaa sio mchezo maana kucheza nae utakiwa kutumia akili, kutakiwa kupiga ngumi za mbali na kutoingia katika staili yake," alisema Kiduku.

Aliongeza kuwa anaamini mkanda huo aliopata utamsaidia kupata mapambano mengine ya kimataifa na hivyo ataendelea kutangaza jina lake.

## Aidani aeleza siri ya mabao

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa JKT Tanzania, Michael Aidan, amesema siri ya yeye kufunga magoli kwa njia ya faulo kutokana na mazoezi anayoyafanya mara kwa mara yeye binafsi, lakini pia na yale anayopewa na kocha mkuu wa timu hiyo, Mohamed Abdallah 'Bares'.

Aidan, ambaye Ijumaa usiku alifunga bao la faulo kwenye mechi dhidi ya Azam, na kuzifanya timu hizo kutoka sare ya bao 1-1, amekuwa na mwendelezo mzuri wa kufunga kwa njia hiyo tangu msimu uliopita.

Ilikuwa ni dakika ya 42, Aidan alipopiga faulo nje kidogo ya eneo la hatari la Azam iliyokwenda moja kwa moja hadi wavuni na kumfanya kipa, David Kisu akiruka baada ya mpira kupita, huku Azam ikisawazisha dakika ya 78 kupitia kwa Salum Aboubakar 'Sure Boy'.

"Ni mazoezi, mimi nafanya sana mazoezi ya kupiga hizi faulo, ndiyo maana sibahatishi, siyo unacheza mpira halafu faulo inatokea ndiyo unapiga, inatakiwa uwe umezifanyia sana mazoezi," alisema Aidan ambaye si mara ya kwanza kufunga magoli kwa staili hiyo.

Beki huyo alisema pamoja na yeye mwenyewe kufanya mazoezi, lakini kocha wake Bares amekuwa msaada mkubwa kwake, kwa sababu humwongezea baadhi ya mbinu ili kupiga faulo kwa ufundi zaidi.

"Ndiyo maana uliona nilipofunga bao nilikwenda kwa kocha wangu, kumpongeza na yeye pia kwa kazi nzuri anayoifanya kwangu," alisema.

Kutokana na sare hiyo ya bao 1-1, JKT Tanzania imefikisha pointi tisa baada ya kushuka dimbani mara tisa, huku Azam ikifisha pointi 22 ikiwa pia imecheza michezo tisa.

## Julio atamani mechi za kirafiki

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), Jamhuri Kihwelo 'Julio', amesema anatamani kupata mechi nyingi za kirafiki ili kukiimarisha kikosi chake kinachotarajia kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika hivi karibuni jijini Arusha.

Julio alisema mechi mbili watakazocheza dhidi ya 'ndugu' zao wa Zanzibar, bado hazitoshi kuwaweka vyema wachezaji wake lakini anaamini watafanya vizuri kwenye michuano hiyo.

Kocha huyo alisema muda uliopo ni mdogo, hivyo ni ngumu timu hiyo kupata michezo mingi ya kirafiki ya kimataifa kama ambavyo alitarajia.

"Kitu pekee ambacho kinanipa moyo na nguvu ni kuwa wachezaji wengi wa U-20 sasa hivi wameshapevuka na wanapata nafasi ya kucheza katika mechi za Ligi Kuu Bara, zinawasaidia kuwajenga na kuwaimarisha," alisema Julio.

Aliongeza muda mfupi atakaokuwa na wachezaji hao, atautumia kutengeneza muunganiko na kufahamu kwa karibu uwezo wa kila mchezaji.

Mashindano ya Cecafa U-20 yanatarajiwa kufanyika hapa nchini kuanzia Novemba 20 hadi Desemba 10 jijini, Arusha.

Michezo
Jumapili Novemba 1, 2020
Nipashe



Pires ampeleka Mbappe Madrid

HABARI UK 22

# Azam FC yalia kukosa bahati

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema timu yake haikuwa na bahati ya kuondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa juzi usiku na kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Vivier aliliambia gazeti hili washambuliaji wake hawakuwa makini katika kutumia vyema nafasi walizozipata katika mchezo huo wa raundi ya tisa.

Kocha huyo alisema timu yao ilicheza vizuri na kuwazidi wapinzani wao lakini amekiri bahati haikuwa upande wao kwa siku ya juzi.

"Kasi ya mechi saba zilizopita ilikuwa juu sana kulingana na wapinzani ambao tumekutana, isipokuwa mechi ya nane na tisa matokeo hayakuwa mazuri kwa sababu ya upungufu yetu, hasa katika kumalizia nafasi za mwisho tunazozipata.

**"Baada ya kupoteza pointi nne, sisi benchi la ufundi na wachezaji wa ujumla kila mechi tunaichukulia kama fainali yetu, ni jukumu letu kuandaa vizuri kila kitu ili kuhakikisha timu inapata pointi tatu, tuna heshimu kila tutakayekutana naye katika ligi hii," alisema Vivier.**

Naye kiungo wa timu hiyo, Salum Aboubakar 'Sure Boy', alisema miaka yote kikosi chao huwa na wakati mgumu wanapokutana na JKT Tanzania na katika mechi hiyo walikutana na ushindani mkubwa.

"Tunashukuru Mungu kupata pointi muhimu, tumefanya makosa wenzetu wameyatumia na kuanza kupata bao lakini na sisi tumetumia makosa yao kusawazisha, ligi bado ndefu tuna imani ya kufanya vizuri mechi zijazo pia kuna upungufu wetu benchi la ufundi litafanyia kazi kuelekea mechi zetu zijazo," alisema Sure Boy.

JKT Tanzania ndio walitangulia kupata bao dakika ya 43 kupitia nyota wake, Michael Aidan kwa mpira wa adhabu na dakika 78 Azam ilisawazisha kupitia Sure Bo.

Kwa matokeo hayo, Azam imeendelea kuongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 22 baada ya kucheza mechi tisa.



Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Mwadui, Jackson Shiga, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 5-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA SC YAZINDUKA, YANGA HAIKAMATIKI

●●●Ni baada ya Mnyama kuisulubu Mwadui, huku Yanga ikipata ushindi wa kwanza Musoma...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO matano yaliyofungwa na wachezaji Watanzania yaliwafanya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, kumaliza hasira za kupoteza mechi mbili mfululizo, ilipoirarua Mwadui FC magoli 5-0 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Wakati Simba ikiishindilia Mwadui idadi hiyo ya mabao, Yanga iliendeleza wimbi la ushindi baada ya kuichapa Biashara United bao 1-0 kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma mkoani Mara.

Nahodha John Bocco alifunga mabao mawili, Ibrahim Ajibu, Hassan Dilunga na Saidi Ndemla waliwafanya wanachama na mashabiki wa Simba jana kutembea kifua mbele baada ya kupoteza mechi mbili mfululizo dhidi ya Prisons na Ruvu Shooting.

Baada ya kosakosa nyingi za Simba, ilifanikiwa kupata bao la kwanza dakika ya 24 lililofungwa na Bocco akimaliza pasi safi iliyopigwa na Clatous Chama ambaye baadaye alikabidhiwa unahodha baada ya mshambuliaji huyo kutoka nje.

Shambulizi pekee kali la Mwadui kwenye mchezo wa jana lilikuwa ni dakika ya 44, baada ya mabeki wa Simba kumsahau Deogratius Antony aliyeingia ndani ya eneo la hatari na kuachia shuti lililotoka nje kidogo ya lango.

Kipa wa Simba, Beno Kakolanya jana alionekana kuwa likizo kwa muda mrefu, kwani alikuwa akidaka mipira hafifu au ile anayorudishiwa na wachezaji wenzake. Bao moja la Simba lilidumu hadi mapumziko kiasi kwamba wengi wakidhani hata kama ikishinda, basi itakuwa ni ushindi kiduchu.

Mabadiliko yaliyofanywa na Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck ya kumtoa Bocco na kumwingiza Ajibu, Rarry Bwalya na kuingia Dilunga na Francis Kahata akichukua nafasi ya Chama, yaliisaidia Simba na kupata mabao manne kipindi cha pili.

Bocco alifunga bao la pili dakika ya 64 akiunganisha krosi ya Ajibu.

Ilipofika dakika ya 81, ndipo balaa kwa Mwadui lilipoanza, ambapo Ajibu alifunga bao la tatu, dakika tano baadaye Dilunga alipachika bao la nne baada ya kumzidi ujanja, Gerald Mgeveke na kuujaza wavuni, huku Ndemla akipigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la Mwadui dakika ya 90 kwa kufunga bao la tano.

Lilikuwa ni bao la 11 kwa Mwadui kufungwa kwenye mechi mbili, mchezo uliopita Mwadui ilichapwa mabao 6-1 dhidi ya JKT Tanzania Jumapili iliyopita nyumbani kwao.

Kwenye Uwanja wa Karume Musoma, Yanga ilipata ushindi wake wa kwanza kwenye uwanja huo baada ya misimu miwili, kwa kuichapa Biashara United bao 1-0, shukrani kwa Mghana Michel Sarpong aliyefunga kwa kichwa akiunganisha krosi ya Ditram Nchimbi dakika ya 68.

Inakuwa ni mara ya kwanza kwa Biashara kupoteza mechi kwenye uwanja huo msimu huu, lakini Yanga inaifunga Biashara United kwa mara ya kwanza tangu ianze kucheza Ligi Kuu Bara msimu wa 2018/19.

Kwa matokeo hayo, Yanga inafikisha pointi 22 sawa na vinara Azam FC yenye uwiano mzuri wa idadi ya magoli wa kufunga na kufungwa wakati Simba yenye pointi 16 imesogea hadi kwenye nafasi ya tatu, lakini vigogo hao wakiwa na mechi mbili pungufu.

Mapema jana mchana Tanzania Prisons ilipoteza mechi nyumbani, kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, baada ya kufungwa bao 1-0 na 'Maafande' wa Polisi, goli likifungwa kwa penalti na Marcel Kaheza.

Ushindi huo unaifanya Polisi Tanzania kufikisha pointi 15 huku Namungo FC ikizinduka usingizini kwa kuichapa Dodoma Jiji bao 1-0 kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi likifungwa na Steven Sey.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Ruvu Shooting kuwakaribisha Coastal Union wakati kesho Mbeya City itawaalika Ihefu FC kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042